ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 29* *26th July, 2024*

*SUBSIDIARY LEGISLATION*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.29 Vol. 105 Dated 26th July, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 630 la tarehe 26/7/2024

SHERIA YA BANDARI,

(SURA YA 166)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 44)*

KANUNI ZA BANDARI ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
TAARIFA ZA CHOMBO

4. Notisi ya kuwasili kwa chombo.
5. Utambuzi wa uzito wa chombo.
6. Ramani za baharini.
7. Mawasiliano na msimamizi wa Bandari.
8. Ishara wakati wa kuingia.

SEHEMU YA TATU
UONGOZAJI WA MELI

9. Mwendokasi wa chombo wakati muongoza meli anapopanda.
10. Uongozaji wa meli wa lazima.
11. Msamaha wa uongozaji wa meli wa lazima.
12. Uongozaji wa meli bandarini.
13. Ngazi ya muongoza meli ya kupanda kwenye chombo.
14. Muongoza meli anatakiwa kuteuliwa.
15. Muongoza meli wa dharura.
16. Majukumu ya muongoza meli.
17. Sifa za muongoza meli.
18. Bendera na mavazi ya muongoza meli.
19. Meli iliyosamehewa kutofungwa kwenye gati iliyopangwa.
20. Uondoaji wa chombo kilichotia nanga katika maeneo ya ndani ya bandari na njia ya kupitia chombo.
21. Ufungaji wa chombo.
22. Uangalizi kuwepo kwenye chombo.
23. Afisa afya bandari.
24. Taratibu za uhamiaji.
25. aratibu za forodha.

SEHEMU YA NNE
UTENDAJI KAZI WA VYOMBO

26. Orodha ya mizigo.
27. Orodha ya vitu vizito.
28. Masharti ya utendaji kazi wa vyombo.
29. Uzuiaji wa shehena na zana za chombo kuanguka bandarini.
30. Utoaji wa taarifa juu ya shehena na zana za chombo zilizoangukia bandarini.
31. Uopoaji wa shehena na zana za chombo zilizoanguka baharini.
32. Nahodha kukitayarisha chombo kwa ajili ya shughuli za shehena.
33. Nahodha kusimamia upakiaji au upakuaji wa shehena.
34. chombo kufanya kazi kulingana na uwezo wake.
35. Stakabadhi ya upokeaji wa shehena.
36. Uwasilishaji shehena kwa Mamlaka.
37. Wakati ambapo shehena inakuwa imepakiwa kwenye chombo.
38. Winchi, trekta za bandari, n.k.
39. Vifaa vya kuhudumia shehena vilivyosimikwa.
40. Makosa yanayohusiana na utumiaji wa winch na n.k.

SEHEMU YA TANO
UHUDUMIAJI WA SHEHENA

41. Gati, ghala na sehemu ya wazi ya kuhifadhi shehena.
42. Uhifadhi wa shehena.
43. Shehena kutokabidhiwa bila kibali.
44. Nyaraka zinazohitajika kabla ya kukabidhi shehena.
45. Bidhaa zilizoingizwa kwa muda.
46. Nyaraka zinazohitajika kusafirisha shehena nje ya nchi.
47. Uwasilishaji au uhifadhi wa shehena kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi.
48. Muda wa kuwasilisha bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi.
49. Kufuta au kurekebisha amri ya usafirishaji.
50. Uwajibikaji unaotokana na ucheleweshaji wa usafirishaji wa bidhaa.
51. Upimaji wa uzito.
52. Uwekaji wa alama kwenye vifurushi.
53. Upelekaji wa bidhaa kwenye ghala la forodha.
54. Vifurushi vyenye kasoro.
55. Ufunguaji wa shehena.
56. Tindikali na dutu zinazofanana na tindikali zilizoletwa katika hali ya kuvuja.
57. Tozo kulipwa kabla au kuwekewa dhamana.

SEHEMU YA SITA
UHUDUMIAJI WA BIDHAA HATARISHI

58. Notisi ya bidhaa hatarishi iliyopo ndani ya chombo.
59. Upakiaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi au zinazoweza kulipuka.
60. Maelekezo ya Mamlaka juu ya bidhaa hatarishi.
61. Ufungaji na uondoshaji wa chombo kilichobeba vilipuzi.
62. Ujazaji wa mafuta katika chombo kilichobeba vilipuzi.
63. Notisi ya upakiaji na upakuaji wa vilipuzi.
64. Masharti mbalimbali kuhusiana na uhudumiaji wa vilipuzi.
65. Ukaguzi na uchunguzi.
66. Utunzaji wa petroli na vimiminika vinavyoweza kuwaka.
67. Utunzaji wa kalisi ya carbide.
68. Uzingatiaji wa sheria na miongozo ya tasnia nyingine.
69. Bidhaa hatarishi zilizoshushwa katika makasha ya ISO.
70. Makosa chini ya Sehemu ya Sita.

SEHEMU YA SABA
SHEHENA YA VIMIMINIKA VINAVYOWEZA KUWAKA

71. Matumizi ya Sehemu hii.
72. Vyeti vya bima na ukaguzi.
73. Hali ya chombo.
74. Uondoaji wa chombo.
75. Usalama wa tanki la mafuta.
76. kufungwa kwa mlango wa sitaha ya Shehena.
77. Upakuaji wa gesi.
78. Kufungwa kwa vali gawanyishi.
79. Masharti ya kupampu.
80. Uhudumiaji wa vimiminika vinavyoweza kuwaka.
81. Makosa chini ya Sehemu ya Saba.

SEHEMU YA NANE
UHUDUMIAJI WA VYOMBO VYENYE MAKASHA

82. Vyombo vyenye makasha kutumia gati maalumu.
83. Usalama wa winchi ya kubeba makasha kwenye gati.
84. Wajibu wa nahodha katika uhudumiaji wa makasha.
85. Vitendea kazi vya chombo kuwekwa tayari.
86. Ufunguaji na ufungaji wa falka kwa chombo kisicho na winchi.
87. Kasha kuwekwa alama.
88. Nahodha au wakala wa chombo kuwasilisha orodha ya shehena.
89. Lakiri ya forodha iliyoidhinishwa.
90. Kupakua kasha kwa ajili ya urahisi wa chombo.
91. Mamlaka kuamua matumizi ya vitendea kazi vya chombo.
92. Kukabidhi au kupokea kasha.
93. Uhamishaji na ufunguaji wa makasha.
94. Kubadilisha hali ya kasha.
95. Ufungaji wa bidhaa usiofaa ndani ya makasha.

SEHEMU YA TISA
UHAMISHAJI, UEGESHAJI WA CHOMBO NA MASUALA YANAOHUSIANA

96. Nahodha mkuu wa bandari kupanga na kusimamia gati.
97. Notisi ya kuhamisha chombo bandarini.
98. Notisi ya ukarabati wa injini.
99. Taa za chombo.

100. Ukodishaji wa stima ya kuvuta chombo.
101. Notisi ya chombo kuondoka.
102. Nanga kuwa tayari kwa kutoswa.
103. Kutoa taarifa ya uharibifu.

SEHEMU YA KUMI
VYOMBO VIDOGO, VYA ASILI NA VYA STAREHE

104. Leseni ya uendeshaji na utiaji nanga wa chombo kidogo cha asili au cha burudani.
105. Kuweka au kuendesha chombo kidogo, cha asili au cha burudani.
106. Ufungaji wa chombo kidogo, cha asili au cha burudanikatika gatini.
107. Ufungaji wa chombo kidogo, cha asili au cha starehe kwa matengenezo.
108. Abiria na mizigo kushushwa sehemu iliyopangwa.
109. Gati la Rais.
110. Nahodha wa chombo kidogo, cha asili au cha burudani kuwasilisha taarifa.
111. Mali ambayo haina mmiliki iwasilishwe kwa Mamlaka.
112. Uwajibukaji juu ya upotevu au majeraha.
113. Zuio kwa vyombo vidogo kupeleka vileo kwa wafanyakazi wa meli.
114. Makosa chini ya Sehemu ya Kumi.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MASHARTI MAALUMU KUHUSIANA NA SHEHENA YA MAJAHAZI

115. Shehena ya majahazi kuhudumiwa katika maeneo yaliyo idhinishwa.
116. Shehena ya jahazi inayoingia na kusafirishwa nje ya nchi.
117. Mamlaka kutowajibika kwa upotevu au uharibifu.
118. Samaki waliokaushwa na kuwekwa chumvi.
119. Uondoshwaji au uuzaji wa bidhaa.
120. Ushughulikiaji au uhudumiaji wa shehena za jahazi.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
UHIFADHI WA SHEHENA

121. Mamlaka inaweza kukataa kuhifadhi baadhi ya shehena.

122. Tozo ya kubadilisha njia ya upakiaji wa bidhaa.
123. Tozo za uhifadhi wa mizigo inayoingizwa nchini.
124. Tozo za mizigo ambayo haijaondolewa katika ghala la Mamlaka.
125. Shehena iliyozuiliwa na Forodha au Polisi.
126. Tozo za uhifadhi wa shehena inayopakiwa kwenda nje ya nchi.
127. Shehena iliyokataliwa.
128. Shehena inayosafirishwa nje ya nchi inaweza kuhamishwa.
129. Uondoshaji wa shehena inayosafirishwa nje ya nchi.
130. Kukosekana kwa eneo la uhifadhi shehena.
131. Msamaha wa tozo za uhifadhi wa shehena
132. Kubadilisha umiliki wa shehena.
133. Tozo za kuhifadhi shehena inayopakiwa kutoka meli moja kwenda meli nyingine na shehena iliyozidi kiwango cha forodha.
134. Mizigo ya abiria ambayo haijaondolewa.
135. Madai ya marejesho ya tozo zilizolipwa zaidi.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## UHIFADHI WA SHEHENA KATIKA GHALA

136. Uhifadhi wa shehena inayosafirishwa nje ya nchi.
137. Tozo maalumu.
138. Uhifadhi wa shehena hatarishi.
139. Ufungashaji wa shehena zilizohifadhiwa ghalani.
140. Utoaji wa taarifa ya shehena na ulipaji wa tozo ya uhifadhi.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## KANUNI ZA JUMLA ZA USALAMA

141. Matumizi ya kanuni za usalama.
142. Wajibu wa Nahodha wa chombo juu ya usalama wa chombo.
143. Tukio la moto.
144. Kupanda au kushuka kwenye chombo.
145. Kutokuacha vitendea kazi vya chombo bandarini.
146. Kutogeuza chombo kwa kutumia injini kikiwa kwenye boya.
147. Katazo la kuwasha moto.
148. Ulevi.
149. Vifaa vya kunyanyua mifuniko ya sitaha.
150. Katazo la kuweka bidhaa kwenye njia.
151. Ukaguzi na majaribio ya mitambo ya kunyanyulia shehena.
152. Mamlaka inaweza kuharibu au kushughulikia shehena kwa namna nyingine.

153. Kibali cha kufanya kazi za moto.
154. Uondoshaji wa mabaki ya gari au chombo.
155. Makosa chini ya Sehemu ya Kumi na Nne.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## USALAMA NA AFYA MAHALA PA KAZI

156. Uzingatiaji wa taratibu na tahadhari za usalama.
157. Uendeshaji wa magari bandarini.
158. Makosa chini ya Sehemu ya kumi na tano.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## UHIFADHI WA MAZINGIRA

159. Katazo la utupaji wa vitu bandarini.
160. Upuliziaji wa dawa ya kuua wadudu kwenye chombo.
161. Cheche, mvuke, masizi, na upakaji rangi.
162. Maji ya farumi.
163. Katazo la umwagaji maji taka.
164. Zuio la uchafuzi na uhifadhi wa mazingira.
165. Miundombinu ya kupokelea taka bandarini.
166. Matumizi ya Mpango wa Mamlaka wa udhibiti taka.
167. Uondoshaji wa chombo bandarini.
168. Udhibiti wa wanyama, ndege, samaki na mimea.
169. Maziko bandarini.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## ULINZI NA UDHIBITI BANDARINI

170. Kufunga barabara na gati.
171. Gari kuegeshwa sehemu iliyopangiwa.
172. Kuingia bandarini bila kibali.
173. Uendeshaji hatarishi.
174. Mwenendo wa madereva bandarini.
175. Uharibifu wa mali za mamlaka.
176. Ishara za hatari.
177. Katazo la maegesho ya gari.
178. Kuwa na kitambulisho au pasi.
179. Kuingia au kutoka katika eneo la bandari.
180. Katazo la kutoa mzigo bila kibali.

181. Ufungaji wa mageti ya bandari.
182. Idhini ya kufanya shughuli ndani ya eneo la bandari.
183. Udhibiti wa wanyama pori na wanyama wasiofugwa.
184. Matumizi ya king'ora.
185. Kibali cha farumi.
186. Katazo la uvutaji wa sigara.
187. Kamati ya ulinzi bandarini.
188. Ulinzi na uingiaji bandarini.
189. Taratibu za uingiaji kwenye maeneo yaliyodhibitiwa.
190. Ukaguzi.
191. Kumzuia afisa wa Mamlaka.
192. Uzingatiaji wa Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Miundombinu ya Bandari.
193. Makosa chini ya Sehemu ya kumi na saba.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## HUDUMA NDOGONDOGO ZA BANDARI

194. Leseni, kibali au makubaliano ya utekelezaji wa shughuli ndogondogo bandarini.
195. Kutoa huduma ndogondogo ndani ya eneo la bandari.
196. Muhudumu wa mizigo bandarini.
197. Ufutaji au usitishaji wa leseni au kibali.

## SEHEMU YA KUMI NA TISA
## MASHARTI YA JUMLA

198. Malipo na tozo za bandari.
199. Makubaliano ya kutoa huduma.
200. Mamlaka ya kutoa miongozo.
201. Adhabu ya jumla.
202. kufutwa.

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA BANDARI,
(SURA YA 166)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 44)*

KANUNI ZA BANDARI ZA MWAKA 2024

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Bandari za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika-
(a) bandari za bahari zilizoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria; na
(b) bandari kavu.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"abiria" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"bidhaa hatarishi" maana yake ni bidhaa zilizoainishwa katika Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi au chapisho jingine lolote la Shirika la Bahari Duniani;

"bandari kavu" maana yake ni kituo cha watumiaji cha pamoja ambacho kimeunganishwa moja kwa moja na bandari kwa reli au barabara yenye miundombinu inayofaa, vifaa na nyenzo za kuhifadhia inayofanya kazi kama kituo cha kupitisha mizigo inayosafirishwa kwa njia ya maji na kontena kwenda na kutoka bandari kavu na inajumuisha bohari ya kupitisha mizigo na makontena matupu;

"cheti cha umahiri" maana yake ni cheti kilichotolewa na Mamlaka au mamlaka nyingine zinazohusika kama itakavyokuwa;

"chombo kidogo" maana yake ni chombo cha kuvutia au kusukuma meli, mashua, jahazi, mashua ya kupiga makasia au chombo chochote kidogo ambacho hakijajumuishwa katika tafsiri ya chombo cha asili;

“eneo la bandari” maana yake ni eneo lililopo ndani ya mipaka ya bandari yoyote kama ilivyotafsiriwa na amri iliyotengenezwa chini ya Sheria;

“eneo la uongozaji wa meli la lazima” maana yake ni eneo la maji linaloruhusu urambazaji wa vyombo lililo ndani ya mipaka ya bandari.

“falka” maana yake ni eneo la wazi katika sakafu ya meli linalotumika kwa madhumuni ya kupakia au kupakua mizigo katika chombo;

“fataki” inajumuisha kutoa ishara au kuokoa Maisha;

“ghala” inajumuisha jengo, sehemu, eneo la wazi lililotengwa, banda na sehemu nyingine yoyote ambapo mizigo inaweza kuhifadhiwa;

“jahazi” inajumuisha vyombo vya majini vya asili, mitumbwi inayotumia mashine, iwe imefungwa injini saidizi au vinginevyo na vyombo vya majini vinavyojiendesha visivyozidi tani zilizosajiliwa 125 au vyenye urefu wa jumla ya mita 38.5 (futi 125), yoyote itakayokuwa kubwa;

“kasha la ISO” maana yake ni kasha kubwa sanifu lililoundwa kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo;

“kituo” maana yake ni miundombinu iliyotengenezwa kwa ajili ya kuhudumia mizigo ambayo inapakiwa au kushushwa na inajumuisha kituo cha abiria, mzigo kichele, makasha au kituo kingine chochote kilichojengwa kwa madhumuni hayo;

“kituo cha makasha” maana yake ni miundombinu iliyotengenezwa kwa ajili ya kuhudumia makasha ya mizigo yanayopakiwa au yanayoshushwa kutoka kwenye vyombo vilivyotengenezwa au kubadilishwa mahususi kwa kusudi hilo;

“Mamlaka” maana yake ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria;

“mipaka ya bandari” maana yake ni eneo lililoko ndani ya mipaka ya bandari yoyote kama inavyoweza kuainishwa kwa amri iliyotengenezwa chini ya Sheria;

“mhudumu wa mizigo bandarini” maana yake ni mtu anayehudumia abiria kwa madhumuni ya kuwasaidia kukamilisha taratibu za mizigo bandarini au ambaye kwa njia yoyote anasimamia

boti au boti ya safu kwa madhumuni ya kusafirisha mizigo ya abiria kwenda au kutoka kwenye meli iliyotia nanga kwenye mkondo;

"meli ya mafuta" maana yake ni meli iliyo na au inayopakia au iliyobeba au inayoelekea kubeba kiasi chochote kikubwa cha shehena ya kimiminika;

"nahodha" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria;

"muongoza meli" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria;

Sura ya 166

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Bandari:

"tozo" maana yake ni fedha zote zinazopokelewa au zinazotozwa na Mamlaka kuhusiana na meli au bandari au uhudumiaji au uhifadhi wa bidhaa ghalani au kuhusiana na huduma nyingine yoyote iliyotolewa au vifaa vilivyotolewa na Mamlaka;

uongozaji wa meli wa lazima" maana yake ni vyombo vya majini vinavyohitaji uongozaji wakati vinapotembea ndani ya mipaka ya bandari;

"ushuru" maana yake ni ushuru na tozo za bandari kama zilivyoainishwa katika kitabu cha tozo;

"Vilipuzi" maana yake ni bidhaa zote zilizoainishwa chini ya Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi Daraja la kwanza; na

"njia ya meli" maana yake ni njia nzima ya urambazaji wa meli au njia ya bandari yoyote.

## SEHEMU YA PILI
## TAARIFA ZA CHOMBO

Notisi ya kuwasili kwa chombo

4.-(1) Mmiliki, nahodha au wakala wa chombo kinachotarajiwa kuwasili bandarini atawasilisha notisi ya kuwasili kwa Mamlaka ndani ya muda usiopungua saa ishirini na nne kabla ya chombo kuwasili.

(2) Notisi itajumuisha taarifa zifuatazo:

(a) tarehe na muda ambao chombo kinatarajiwa kuwasili;
(b) taarifa za chombo;
(c) kusudi la kuwasili;
(d) taarifa za wakala anayewakilisha chombo;
(e) bandari ya mwisho kuwasili;
(f) aina na kiasi cha mizigo itakayopakiwa au

kushushwa;

(g) maelezo ya kina ya vyeti vya usalama na muda wa uhalali wake;

(h) suala lolote linaloweza kuathiri uingiaji salama bandarini na ufungaji wa chombo bandarini au kasoro yoyote kwenye umbo, mashine au kifaa ambayo inaweza-

(i) kuathiri uendeshaji salama wa chombo au usalama wa vyombo vingine; au

(ii) kusababisha hatari kwa mazingira, watu au mali.

(3) Endapo chombo kinachokusudia kuwasili bandarini ni meli ya mafuta, mmiliki, nahodha au wakala wa chombo, pamoja na taarifa zilizoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), atahakikisha kwamba notisi inajumuisha taarifa kuhusu-

(a) aina ya mzigo, jina lake sahihi la kitaalamu, namba iliyotolewa na Umoja wa Mataifa na nyuzi joto ya chini inayoweza kusababisha mlipuko, kama inatumika, na wingi;

(b) mpangilio wa mizigo ndani ya meli inayoonesha mizigo itakayoshushwa au kupakiwa;

(c) kama meli ya mafuta imewekewa mfumo wa gesi na inafanya kazi kikamilifu na ikiwa itawasili ikiwa na gesi au haina gesi;

(d) chombo cha kukinga mafuta yatakayomwagika kutoka kwenye mipira iliyounganishwa chini ya mabomba ya mafuta kimewekwa kwenye manifodi; na

(e) umbali kutoka kwenye manifodi mpaka mbele au nyuma ya meli.

(4) Nahodha Mkuu wa Bandari, kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama, mpangilio, ufanyaji kazi wa bandari unaofaa na wenye ufanisi, anaweza kutoa au kukataa kutoa ruhusa au kuondoa au kubadilisha ruhusa iliyotolewa awali kwa ajili ya chombo chochote kukaribia au kuingia bandarini.

(5) Mmiliki au nahodha wa chombo atawajibika kwa uharibifu wowote au matokeo yanayotokana na taarifa yoyote isiyo sahihi iliyotolewa na yeye mwenyewe au

muwakilishi wake kuhusiana na kina cha meli.

Utambuzi wa uzito wa chombo

5. Nahodha wa chombo pale inapotakiwa, atawasilisha au kutoa kwa Mamlaka cheti cha usajili wa meli kwa madhumuni ya utambuzi wa uzito wa meli.

Ramani za baharini

6. Nahodha wa chombo, kabla ya kuingia au kutembea ndani ya bandari, atahakikisha kuwa analo chapisho la toleo la karibuni la ramani za baharini na chapisho linalohusiana na bandari hiyo.

Mawasiliano na msimamizi wa bandari

7.-(1) Nahodha wa chombo atawasiliana na msimamizi wa bandari au kituo cha Mfumo wa Uongozaji wa Vyombo Baharini pale inapohitajika wakati anapowasili katika safu ya Mawimbi ya Mawasiliano ya Masafa Marefu kwenye chaneli ya 12 au 16.

(2) Chombo kinachoingia bandarini kitazingatia maelekezo yote yaliyotolewa na msimamizi wa bandari au Kituo cha Mfumo wa Uongozaji wa Vyombo Baharini kwenye chaneli ya 12.

Ishara wakati wa kuingia

8. Kabla ya kuingia bandarini, chombo kitaonesha-

(a) bendera yake ya taifa ambayo itapeperushwa kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa 12 jioni;
(b) bendera yenye herufi ya ishara ya meli;
(c) bendera “Q” ambayo haitashushwa mpaka pale afisa afya wa bandari atakapotoa ruhusa;
(d) ikiwa kimebeba abiria, bendera “I” ambayo haitashushwa mpaka afisa wa bandari atakapo taarifiwa ;
(e) ikiwa mifugo itakuwa inapandishwa kwenye chombo hicho, bendera “N” itapandishwa;
(f) ikiwa imebeba bidhaa hatarishi, bendera “B” itapandishwa wakati wa mchana na mwanga mwekundu wakati wa usiku;
(g) bendera ya Tanzania ambayo itapeperushwa kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni;
(h) iwapo muongoza meli atakuwa ndani ya chombo, bendera “H” itapandishwa wakati wa mchana na wakati wa usiku miale miwili ya mwanga mweupe na juu yake mwanga

mwekundu; na

(i) ishara nyingine yoyote kama inavyoweza kuelekezwa na msimamizi wa bandari.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZAJI WA MELI

Mwendokasi wa chombo wakati muongoza meli anapopanda

9. Chombo kitaendeshwa kwa mwendo salama kama itakavyoelekezwa na muongoza meli au msimamizi wa bandari wakati muongoza meli anapanda kwenye chombo na mazingira mazuri kwa ajili ya shughuli za muongozaji yatawekwa.

Uongozaji wa meli wa lazima

10.-(1) Nahodha wa chombo, isipokuwa kama ni chombo kilichosamehewa, hataelekeza au kuruhusu chombo kuingia, kuondoka au kufungwa katika eneo la uongozaji wa lazima wa meli bila kuwa na muongoza meli aliyeteuliwa na Mamlaka ndani ya chombo.

(2) Endapo chombo, isipokuwa chombo kilichosamehewa, kipo katika mazingira ambayo uongozaji wa meli ni wa lazima na hakiko chini ya uongozaji wa meli kama inavyotakiwa na Kanuni hizi, nahodha wa chombo atakuwa anatenda kosa.

(3) Endapo vyombo viwili au zaidi vinakaribia eneo la mipaka ya uongozaji wa meli wa lazima, boti ya muongoza meli itaonesha idadi ya waongoza meli waliopo katika boti hiyo kwa taa ya Aldis au redio ya Mawimbi ya Mawasiliano ya Masafa Marefu.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), ishara zitakazooneshwa na boti ya waongoza meli zitachukuliwa kama tahadhari ya nyongeza kwa chombo ambacho hakina muongoza meli na kitatakiwa kubaki nje ya mipaka ya bandari kama ilivyoelekezwa katika Kanuni hizi.

(5) Mamlaka inaweza kutenga maeneo mengine ndani ya mipaka ya bandari kuwa maeneo ya uongozaji wa lazima wa meli.

Msamaha wauongozaji wa meli wa lazima

11.-(1) Mamlaka, baada ya kupokea maombi kutoka kwa nahodha wa chombo, inaweza kutoa msamaha wa uongozaji wa meli wa lazima kwa chombo chochote au aina ya vyombo.

(2) Endapo chombo kimepewa msamaha kutokana na uongozaji wa lazima wa meli, Mamlaka, baada ya malipo ya ada iliyoelekezwa , itatoa cheti cha msamaha kwa nahodha wa chombo.

(3) Cheti cha msamaha kitaendelea kutumika kwa kipindi cha miezi kumi na mbili kutoka tarehe ya kutolewa, isipokuwa kama kitasimamishwa au kubatilishwa au kama nahodha wa chombo atakoma kuongoza chombo hicho.

(4) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), chombo , kwa ishara au katika tukio maalumu, kinaweza kupewa msamaha wa uongozaji wa meli wa lazima bila kutolewa kwa cheti cha msamaha.

(5) Chombo kilichopewa msamaha wa uongozaji wa lazima wa meli kitaonesha ishara za kimataifa wakati wa kuingia au kutoka bandarini.

(6) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), cheti kitatolewa kwa nahodha wa chombo baada ya kuwasilisha cheti halali cha umahiri na kuonesha uwezo wa kuongoza chombo kwa usalama katika lango la meli kuingilia bandarini.

(7) Nahodha wa chombo ambaye amepewa cheti cha msamaha chini ya Kanuni hizi, baada ya cheti hicho kuisha muda wake, kubatilishwa au kufutwa atakirudisha kwa Mamlaka iliyokitoa.

Uongozaji wa meli bandarini

12.-(1) Chombo, chombo cha asili au chombo kidogo kinachowasili bandarini, isipokuwa chombo kilichosamehewa-

(a) kitasubiri kuwasili kwa boti ya waongoza meli kwenye eneo la nje la kutia nanga; na
(b) kitatia nanga nje ya alama za kuongozea vyombo, endapo ni lazima.

(2) Maelekezo ya uongozaji wa chombo yatawasilishwa kwa redio ya Mawimbi ya Mawasiliano ya Masafa Marefu au kwa ishara kutoka kituo cha usimamizi au Mfumo wa Uongozaji wa Vyombo Baharini au kwa njia nyingine yoyote ya mawasiliano inayofaa .

Ngazi ya muongoza meli ya kupanda

13. Nahodha wa chombo atahakikisha kwamba ngazi ya muongoza meli ya kupanda kwenye chombo inazingatia yafuatayo:

kwenye chombo

(a) inawekwa katika hali ya usafi na kwa utaratibu mzuri na inatumiwa na maafisa au watu wengine walioidhiniwa wakati meli inapowasili au kuondoka bandarini na kwa ajili ya waongoza meli kupanda au kushuka kwenye chombo;

(b) inawekwa katika hali ambayo kila hatua kwenye ngazi inaegemea kwa uthabiti upande wa meli kwa ajili ya mtu anayeitumia aweze kufika kwa urahisi na salama kwenye meli baada ya kupanda kwa umbali usiopungua mita 1.5 (au futi 5) na usiozidi mita 9 (au futi 30);

(c) urefu mmoja wa njia ya nahodha ya kufika melini na posho utazingatiwa wakati wote wa upakiaji na upunguzaji wa meli;

(d) endapo meli ina umbo lenye urefu wa zaidi ya mita 9 kutoka kwenye sakafu ya meli mpaka usawa wa maji , ngazi iliyounganishwa itatumika;

(e) imethibitishwa kwa mujibu wa kanuni ya 23 ya Sura ya V ya SOLAS.

muongoza meli anatakiwa kuteuliwa

14.-(1) Mtu yeyote hatatoa huduma kama muongoza meli isipokuwa muongoza meli aliyeteuliwa au muongoza meli wa dharura aliyeteuliwa na Mamlaka chini ya kanuni ya 15.

(2) Uteuzi wa muongoza meli utakuwa kama ulivyoainishwa katika mwongozo wa uendeshaji wa bandari.

Muongoza meli wa dharura

15. Mamlaka inaweza kuidhinisha mtu mwingine asiyekuwa muongoza meli aliyeteuliwa kuongoza meli kama hatua za muda mfupi na za dharura endapo kutakuwa na uhaba wa watumishi.

Majukumu ya muongoza meli

16. Kwa kuzingatia maelekezo ya Mamlaka, majukumu ya muongoza meli yatajumuisha-

(a) kuendesha chombo bandarini kwa kuelekeza mienendo yake, kuamua na kudhibiti mienendo ya boti inayosaidia chombo kilicho chini ya uongozaji; na

(b) kuainisha idadi ya boti za kusaidia meli zinazohitajika kwa ajili ya kuongozea meli kwa maelewano na nahodha wa chombo:

Isipokuwa kwamba, endapo kutatokea kutoelewana kati ya muongoza meli na nahodha wa chombo kuhusu idadi ya boti za kusaidia meli zitakazotumika, Nahodha Mkuu wa Bandari atatoa uamuzi wa mwisho.

Sifa za Muongoza meli

17.-(1) Mtu tofauti na muongoza meli aliyeteuliwa kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, hatateuliwa kuwa muongoza meli isipokuwa kama ana sifa zifuatazo:

(a) ni mtu mwenye umri usiopungua miaka ishirini na tano na usiozidi miaka arobaini na tano;
(b) ni mtu mwenye vyeti kuhusiana na uwezo na utimamu wake kwa ajili ya uteuzi huo, ikiwa ni pamoja na cheti cha afya kinachoonesha kwamba ana afya njema na hasumbuliwi na udhaifu wowote wa mwili unaomfanya kuwa mtu asiyefaa kutekeleza majukumu ya muongoza meli;
(c) ameiridhisha Mamlaka juu ya ujuzi wake wa ubaharia;
(d) ana angalau cheti cha umahiri cha Afisa Mwendesha Meli Daraja la Pili; na
(e) ana angalau cheti cha umahiri cha Afisa Mwendesha Meli Daraja la Tatu;

Isipokuwa kwamba, mtu mwenye cheti cha Daraja la Tatu hataongoza vyombo vya majini vyenye uzito wa zaidi ya tani 7000.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1)(c), afisa mwendesha meli Daraja la Tatu mwenye cheti cha umahiri anaweza kuteuliwa kama muongoza meli baada ya kuthibitishwa na Mamlaka yenye dhamana ya uongozaji wa meli.

Bendera na mavazi ya muongoza meli

18.-(1) Mtu tofauti na muongoza meli aliye majini na aliye zamu hataruhusiwa kupandisha bendera ya muongoza meli, nusu nyeupe juu, nusu nyekundu chini.

(2) Mamlaka itahakikisha kuwa waongoza meli wanapatiwa mavazi kulingana na vyeo vyao.

Meli iliyosamehewa kutofungwa kwenye gati iliyopangwa

19. Meli iliyosamehewa, ikiwa haijafungwa kwenye gati iliyopangiwa na Mamlaka, na ambayo imeonekana kuharibu au ina uwezekano wa kuharibu alama yoyote, boya, boya la kushikilia meli au vyombo vingine vya majini kwa sababu ya kutofungwa kwa umadhubuti au sababu nyingine, inaweza kuhamishwa au kufungwa kwa maelekezo ya Nahodha Mkuu wa Bandari.

Uondoaji wa chombo kilichotia nanga katika maeneo ya ndani ya bandari na njia ya meli

20.-(1) Mamlaka, pale ambapo meli, chombo cha asili au chombo kidogo, kimetia nanga katika eneo lolote la ndani ya bandari ya ndani au njia ya kupitia meli bila idhini ya Nahodha Mkuu wa Bandari, inaweza kuondoa meli hiyo, chombo cha asili au chombo kidogo kwa gharama za mmiliki au nahodha.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), endapo chombo kimeondolewa chini ya usimamizi wa muongoza meli, tozo kamili ya uongozaji wa meli itatatozwa na, endapo Mamlaka itaona kuwa kuna umuhimu wa matumizi ya boti ya kusukuma meli, pia tozo za uvutaji chombo zitatozwa.

Ufungaji wa chombo

21. Kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chombo, nahodha wa chombo atahakikisha kuwa-

(a) chombo kilicho ndani ya bandari wakati wote kina watumishi wa kutosha kwa ajili ya kufunga chombo hicho na kuweka ngazi ya kupandia na njia za kutokea chomboni kufika nchi kavu ili kuhakikisha usalama wa chombo;
(b) kamba za kufungia chombo hazitachukuliwa kuwa zimefungwa kwa umadhubuti isipokuwa kama zimefungwa kwenye nguzo za kufungia meli za ndani ya maji zilizowekwa kwa ajili hiyo, na kamba ya waya haitatumika isipokuwa kama nguzo ya kufungia meli na ukingo wa kushikilia gati umekingwa dhidi ya msuguano kwa kiwango cha kumridhisha Nahodha Mkuu wa Bandari;
(c) minyororo haitumiki kwa ajili ya kufungia meli, isipokuwa kwa idhini ya Nahodha Mkuu wa Bandari;
(d) meli inatia nanga, inawekwa na kufungwa

kwenye gati kwa kiwango cha kumridhisha Nahodha Mkuu wa Bandari na meli hiyo itachukua tahadhari za ziada katika hali mbaya ya hewa kama itakavyoamriwa; na

(e) meli iliyofungwa kwenye gati inaweka vilinda panya vya kutosha kwenye kila mstari na waya uliounganishwa au unaofika ufukweni:

Isipokuwa kwamba, katika mazingira ambayo hakuna watumishi wa kutosha ndani ya meli, Mamlaka itatoa wafanyakazi wengine kwa gharama ya mmiliki au nahodha wa chombo ambayo itatozwa kwa mujibu wa Kitabu cha Tozo cha Mamlaka.

Uangalizi kuwepo kwenye chombo

22.-(1) Nahodha wa chombo atafanya uangalizi kwenye sitaha ya meli mchana na usiku wakati meli iko bandarini.

(2) Bila kujali katika kanuni ndogo ya (1), nahodha wa chombo, wakati wa dharura na kwa idhini ya Mamlaka, anaweza kuajiri mtu mwingine kwa ajili ya uangalizi.

Afisa afya wa bandari

23.-(1) Chombo kinachoingia bandarini kitasubiri kuwasili kwa afisa afya wa bandari kabla ya kuwasiliana na watu walio nchi kavu au na meli nyingine au boti isipokuwa muongoza meli au boti ya afisa wa Forodha.

(2) Mamlaka itahakikisha kuwa afisa afya wa bandari anapewa taarifa kuhusu kuwasili kwa chombo.

Taratibu za uhamiaji

24.-(1) Afisa afya wa bandari anaweza kutoa ruhusa kwa meli kuingia bandarini kwa ajili ya afisa uhamiaji kuanza taratibu za kutoa kibali cha kuingia bandarini.

(2) Mtu hatatoka kwenye chombo kabla ya kukamilika kwa taratibu za kibali cha kuingia bandarini isipokuwa kwa ruhusa ya afisa uhamiaji.

Taratibu za Forodha

25. Mtu hatatoka nje ya eneo la bandari kabla ya kukamilika kwa taratibu za kuingia bandarini isipokuwa kwa kibali cha maandishi kilichotolewa na Afisa Forodha.

## SEHEMU YA NNE
## UTENDAJI KAZI WA VYOMBO VYA MAJINI

Orodha ya mizigo

26.-(1) Wakala wa chombo atawasilisha orodha ya mizigo kwenye mfumo uliopo angalau siku saba kabla ya kuwasili au kuanza kufanyiwa kazi kwa chombo bandarini.

(2) Orodha ya mizigo iliyorejewa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha-

(a) maelezo ya chombo, namba ya safari, na tarehe inayotarajiwa ya kuwasili na kuondoka;

(b) nchi ya asili ya chombo kilipotoka na kituo cha chombo kinapokwenda; na

(c) bandari kilipopakia, kitakaposhushia, na sehemu kitakapopita wakati wa safari.

(3) Kwa mizigo iliyowekwa kwenye makasha, mizigo kichele na mizigo mikubwa, orodha ya mizigo itajumuisha-

(i) jina la mtumaji na mpokeaji wa shehena, anwani na taarifa za mawasiliano;

(ii) jina, anwani na maelezo ya mawasiliano ya wakala wa mizigo;

(iii) mkataba wa usafirishaji wa shehena au stakabadhi;

(iv) alama na namba za mizigo;

(v) namba na maelezo ya vifungashio au bidhaa;

(vi) maelezo ya mizigo iliyobebwa na chombo; na

(vii) uzito wa chombo.

(4) Chombo hakitaanza kushusha mizigo mpaka pale orodha kamili ya mizigo itakapowasilishwa kwa Mamlaka.

(5) Wakala ataiarifu mamlaka husika na kulipa ada zilizowekwa endapo kuna marekebisho yoyote yatakayofuata kwenye orodha ya mizigo.

Orodha ya vitu vizito

27. Wakala wa meli, wakati wa kuwasilisha orodha ya mizigo, ataweka kwenye mfumo unaotumika orodha ya vitu vyenye uzito wa zaidi ya tani tano vilivyomo kwenye shehena itakayoshushwa bandarini.

Chombo kutia nanga

28.-(1) Chombo kitapangiwa kufungwa gatini kwa kuzingatia mpangilio wa kuwasili kwake au kwa kuzingatia utashi wa Mamlaka.

(2) Mamlaka haitakihakikishia kukifanyia kazi chombo chochote kilichopo kwenye eneo la kutia nanga isipokuwa pale ambapo hali ya hewa na hali nyingine inaruhusu.

(3) Mamlaka inaweza kukataa kuruhusu mizigo kushushwa kutoka kwenye chombo chochote mpaka litakapopatikana gati, banda au eneo jingine linalofaa la kuhifadhia mizigo hiyo .

(4) Mamlaka haitaruhusu mizigo yoyote kushushwa isipokuwa kama masharti kuhusu uunganishaji wa mizigo, uwekaji wa alama au vyote kwa pamoja ufangamanishaji wa mizigo na uwekaji wa alama vimezingatiwa.

(5) Mamlaka haitawajibika kwa hasara, uharibifu, ucheleweshaji au kutokutolewa kwa mizigo kulikosababishwa na kutokuzingatia masharti yaliyotajwa chini ya kanuni hii.

Uzuiaji wa shehena na zana za chombo kuanguka bandirini

29.-(1) Nahodha wa chombo kinachopakia au kushusha mizigo atahakikisha kuwa hatua zote zinachukuliwa kwa ajili ya kuzuia mizigo au zana za chombo kuanguka bandarini.

(2) Mamlaka haitawajibika iwapo hatua hazijachukuliwa kwa ajili ya kuzuia mizigo au zana za chombo kuanguka bandarini.

Utoaji wa taarifa juu ya shehena na zana za chombo zilizoangukia bandarini

30. Nahodha wa chombo atatoa taarifa kwa Mamlaka ndani ya muda wa kazi kuhusiana na mizigo au zana za chombo zilizoangukia baharini na atatoa maelezo mengine yoyote ambayo Mamlaka inaweza kuhitaji.

Uopoaji wa shehena na zana za chombo zilizoanguka bandarini

31.-(1) Nahodha wa chombo atawezesha shehena au zana za chombo zilizoangukia baharini kutolewa humo kabla ya meli kuondoka na atazingatia maelekezo ya Mamlaka kuhusu utoaji huo.

(2) Endapo Nahodha wa Chombo atashindwa kutoa mizigo au zana za chombo zilizoangukia bandarini, Mamlaka inaweza kutoa mizigo au zana hizo, na mmiliki

au nahodha wa chombo atawajibika kulipa gharama zinazotokana na urejeshaji wa mizigo au zana za chombo zilizoangukia bandarini.

(3) Mwendeshaji wa kituo au mtoa huduma za bandari atahakikisha kuwa mizigo, uhudumiaji wa mizigo, vifaa vya kufungashia au mafuta yaliyomwagika ambayo yameangukia kwenye gati au sehemu yoyote ya bandari yanaondolewa, na endapo hayataondolewa, Mamlaka itaweka utaratibu wa kuyaondoa kwa gharama za mtu anayehusika.

Nahodha kukitayarisha chombo kwa ajili ya shughuli za shehena

32. Nahodha atatayarisha chombo kwa ajili ya shughuli za shehena kwa kiwango cha kuiridhisha Mamlaka au mwendeshaji mwingine aliyeteuliwa.

Nahodha kusimamia upakiaji na upakuaji wa shehena

33.-(1)Nahodha au mtu mwingine mwenye dhamana aliyeteuliwa naye, atakaa ndani ya chombo wakati wa upakiaji au upakuwaji wa shehena kwa madhumuni ya kusimamia upakiaji au upakuaji huo.

(2) Nahodha wa chombo atawajibika kulipia gharama za uharibifu wowote utakaosababishwa na mpakizi au mpakuzi wakati wa shughuli hizo.

chombo kufanya kazi kulingana na uwezo wake

34.-(1) Endapo chombo kitashindwa kupakia au kushusha mizigo yake kwa namna inavyoonekana inafaa kwa Mamlaka, chombo hicho kitapoteza zamu yake ya kupakia au kushusha mizigo yake na kinaweza kuondolewa na Mamlaka kwa hatari na gharama za mmiliki wa chombo.

(2) Endapo mtambo au nguvu kazi iliyoandaliwa kwa madhumuni maalumu ya kushusha, kusafirisha au kuhamisha mizigo haitatumika kikamilifu kutokana na matatizo ya chombo, gharama zilizotumika zitalipwa na mmiliki wa chombo.

(3) Mamlaka itakitaka chombo kusimamisha upakuaji au kupunguza kiwango cha upakuaji wa mizigo iwapo kutatokea mlundikano wa bidhaa kwenye gati, au eneo la pembezoni mwa gati, au kwenye gati la vyombo vidogo, au kwa sababu yoyote itakayoonekana inafaa..

Stakabadhi ya upokeaji wa shehena

35. Mamlaka, baada ya kila kitu kushushwa kwa utaratibu, na kuwekewa alama ipasavyo, itatoa stakabadhi kwa nahodha au wakala wa chombo, kwa mizigo yote iliyopokelewa, isipokuwa kama wamekubaliana vinginevyo kati ya Mamlaka na nahodha au wakala wa chombo:

Isipokuwa kwamba, endapo mizigo itashushwa na Mamlaka kwa namna ambayo inazuia uchukuaji wa hesabu sahihi ya mizigo wakati wa kuishusha, stakabadhi itatolewa baada ya kupanga na kuweka mizigo hiyo ufukweni na hapo ndipo itachukuliwa kuwa utoaji wa mizigo hiyo kwa Mamlaka umefanyika.

Uwasilishaji wa shehena kwa Mamlaka

36.(1) Uwasilishaji wa mizigo hautachukuliwa na Mamlaka kuwa umefanyika hadi pale mzigo utakaposhushwa salama kwenye gati au gati ya vyombo vidogo na kuondolewa kwenye chombo cha kuhudumia mizigo kilichotumika kushushia mzigo huo.

(2) Kwa Chombo cha RoRo, bidhaa zitachukuliwa kuwa zimeshushwa na kukabidhiwa kwa Mamlaka baada ya mizigo au bidhaa ikijumuisha makasha ya ISO kuondolewa kwenye daraja la kushushia magari.

Wakati ambapo shehena itakuchuliwa kuwa imepakiwa kwenye chombo

37.-(1) Bidhaa kwa ajili ya kusafirishwa zitachukuliwa kuwa zimefikishwa na Mamlaka kwenye meli ipasavyo kwa utaratibu na hali nzuri baada ya kuwekwa kwenye kifaa cha kubebea mizigo kilicho pembeni ya meli iliyo kwenye gati au kwenye gati ya vifaa vidogo, isipokuwa kama kuna makubaliano tofauti, au kama bidhaa hizo zimekataliwa na meli na zimeharibika au ziko katika hali mbaya.

(2) Bidhaa zikijumuisha makasha ya ISO wakati zinasafirishwa zikiwa juu ya daraja la kushushia magari zitachukuliwa kuwa zimesafirishwa na kuwasilishwa wakati ambapo magurudumu ya mbele ya gari yanapogusa daraja la kushushia magari.

Winchi, trekta za bandari, n.k

38.-(1) Nahodha wa chombo kinachotaka kupakua au kupakia bidhaa kwenye ukingo wa gati au gati ambapo winchi, trekta ya kuhudumia mizigo au vifaa vingine vinavyoendeshwa vimetolewa na Mamlaka na iwapo

atatakiwa na Mamlaka, atatumia kifaa kwa kulipa ada kwa viwango vilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo na masharti yafuatayo yatatumika:

(a) tozo itatatozwa kuanzia muda uliotajwa katika maombi, yaliyowasilishwa na nahodha au wakala wa chombo kwa Mamlaka, au, ikiwa winchi au trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au kifaa kingine hakiko tayari, kuanzia muda kitakapokuwa tayari au kitakapopatikana;

(b) mtu anayetumia winchi hatapitisha kamba, waya au mnyororo chini ya ukingo wa falka na mizigo haitavutwa kutoka chini au juu ya sitaha kwa kamba za waya za winchi;

(c) Mamlaka haitawajibika kwa hasara yoyote, uharibifu au ajali inayoweza kutokea katika ufanyaji kazi wa winchi au trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au vifaa vingine;

(d) mtu anayetumia winchi au mwendeshaji wa bandari atazingatia amri au masharti yoyote yanayofaa kuhusiana na ufanyaji kazi au kusimamishwa au ufanyaji kazi wa winchi na trekta ya kuhudumia mizigo bandarini ambayo yanaweza kutolewa au kuwekwa na Mamlaka;

(e) gharama ya matumizi ya winchi, trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au vifaa vingine kwenye mabanda ya kuhifadhia mizigo inayosafirishwa au sehemu ya kupangia mizigo italipiwa na mtu anayehitaji kutumia vitu hivyo kwa viwango vilivyoainishwa na Kitabu cha Tozo cha Mamlaka; na

(f) Mamlaka inapotoa winchi iliyosimama au inayotembea kwa madhumuni ya kunyanyua mizigo mizito, ikiwa ni tani 5 au zaidi kwa kila kipande au kifurushi, uhalibifu utakaosababishwa kwenye au na vipande au vifurushi vyovyote vilivyonyanyuliwa hautakuwa juu ya Mamlaka.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) (c), endapo winchi au trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au vifaa vingine vinafanyiwa kazi na mtumishi

wa Mamlaka, mtu atakayepewa ruhusa ya kutumia winchi au trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au vifaa vingine atawajibika kwa uharibifu wowote utakaotokea katika winchi au trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au vifaa vingine au kwenye zana inayohusiana nayo, au kwa mali yoyote, kwa wakati huo zinapotumiwa na mtu huyo, isipokuwa hatawajibika kwa uchakavu wa kawaida.

Vifaa vya kuhudumia shehena vilivyosimikwa

39. Chombo kilichofungwa karibu au chini ya vifaa vya kuhudumia mizigo vilivyosimikwa kitakuwa na wafanyakazi wa kutosha ndani ya chombo tayari kwa kuhamisha chombo hicho saa yoyote, mchana au usiku, kama au wakati itakapoelekezwa na Nahodha Mkuu wa Bandari.

Makosa yanayohusiana na utumiaji wa winchi, n.k

40. Mtu anayetumia winchi, trekta ya kuhudumia mizigo bandarini au vifaa vingine, kwa madhumuni mengine tofauti na shughuli za uendeshaji wa bandari anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi Dola za Marekani mia mbili au kiasi sawa na hicho katika Shilingi za Tanzania au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote.

## SEHEMU YA TANO
## USHUGHULIKIAJI WA SHEHENA

Ghala, gati na sehemu ya wazi ya kuhifadhi shehena

41. Mtu hataruhusiwa kuingia kwenye ghala, gati na sehemu ya wazi ya kuhifadhia shehena ndani ya eneo la bandari kwa ajili ya utoaji, upakiaji na upakuaji isipokuwa kama ameidhinishwa na Mamlaka.

Uhifadhi wa shehena

42.-(1) Mamlaka itatenga eneo kwa ajili ya kuhifadhi shehena.

(2) Iwapo kutakuwa na kumwagika kwa shehena, Mamlaka itaifunga tena shehena hiyo na mteja atalipa gharama za ufungaji upya wa shehena kama ilivyoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

Shehena kutokabidhiwa bila kibali

43.- Mamlaka haitakabidhi shehena kwa mpokeaji wa shehena yeyote bila kibali kutoka idara ya Forodha.

Nyaraka zinazohitajika kabla ya kukabidhi shehena

44.-(1) Kabla ya kukabidhiwa shehena mpokea shehena au wakala atawasilisha kwa Mamlaka nyaraka zifuatazo:

(a) nyaraka ya utoaji wa shehena, ikiwa imejazwa kila kipengele kwa kuainisha alama na nambari husika za vifungashio, au taarifa kuhusiana na bidhaa ambazo hazipo katika vifungashio, idadi yake, maelezo na yaliyomo pamoja na uzito, kipimo cha ujazo, jina la chombo, tarehe ya kuwasili na maelekezo ya uondoshaji;

(b) hati ya mzigo na hati ya kukabidhi mzigo ya msafirishaji, iliyotolewa na mawakala wa chombo; na

(c) kibali cha kutoa shehena cha idara ya forodha.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1), hayatatumika kwa malipo ya shehena ambayo imetathminiwa kwa misingi iliyoainishwa katika Kitabu cha Tozo, ambapo, kipimo cha uzito au ujazo kitakuwa kwa mujibu wa vipimo vilivyotajwa katika Kitabu cha Tozo au hati ya kusafirishia shehena..

Bidhaa zilizoingizwa kwa muda

45. Bidhaa kwa ajili ya uchunguzi wa forodha ambazo ziko chini ya ingizo la muda hazitachukuliwa kuwa zimeondolewa hadi hapo uingizaji rasmi utakapofanyika.

Nyaraka zinazohitajika katika kusafirisha shehena nje ya nchi

46.-(1) Mtu anayekusudia kusafirisha shehena atawasilisha nyaraka ya upakiaji shehena kwa Mamlaka kupitia mfumo uliopo, na iwapo kuna shehena tofauti tofauti kutakuwa na nyaraka ya upakiaji shehena kwa kila shehena.

(2) Mamlaka haitosafirisha shehena kutoka kwenye ghala la bandari kwenda kwenye chombo isipokuwa kama imepokea nyaraka ya upakiaji wa shehena husika.

Uwasilishaji au uhifadhi wa shehena kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi

47.-(1) Mtu hataweka au kuleta shehena yoyote kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi katika bandari yoyote bila maelekezo kutoka kwa Mamlaka.

(2) Mmiliki wa shehena yoyote iliyoletwa au iliyowekwa kwa kukiuka kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya Dola

kumi za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa shilingi za Tanzania kwa siku kwa kila tani moja au Dola za Marekani mia mbili kwa kila ujazo wa kasha lenye urefu wa futi ishirini (TEU) kwa siku hadi shehena itakapoondolewa.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (2), Mamlaka inaweza kuondoa bidhaa kwa gharama za mmiliki.

Muda wa kuwasilisha bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi

48.-(1) Bidhaa zinazokusudiwa kusafirishwa na chombo chochote mahsusi pamoja na nyaraka husika za agizo la upakiaji wa bidhaa zitawasilishwa sehemu iliyotengwa ndani ya bandari ndani ya saa kumi na mbili za kazi kabla ya chombo kuwasili.

(2) Endapo bidhaa au nyaraka za agizo la upakiaji wa bidhaa zitapokelewa kwa kuchelewa, msafirishaji atawajibika kwa gharama zozote za ziada zitakazotumika.

(3) Bidhaa ambayo nyaraka zake za agizo la upakiaji zimewasilishwa zitakuwa tayari kusafirishwa kwa kila namna na msafirishaji au mtu mwingine yeyote anayehusika kwa namna itakavyokuwa.

(4) Bidhaa hazitapangwa upya au kurekebishwa ndani ya eneo la bandari isipokuwa kama idhini imetolewa na Mamlaka.

(5) Bidhaa ambazo hazifai kusafirishwa zitaondolewa bandarini ndani ya saa arobaini na nane tangu kugundulika kwa hali hiyo.

(6) Bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi hazitapokelewa na Mamlaka isipokuwa kwa ajili ya kuhifadhiwa ghalani, na baada yakulipiwa tozo zilizoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

Kufuta au kurekebisha amri ya usafirishaji

49.-(1) Amri ya kufuta au kurekebisha nyaraka za agizo la upakiaji wa bidhaa la awali kutoka kwa mtu mwenye udhibiti halali wa bidhaa, inaweza kukubaliwa na Mamlaka baada ya kuwasilishwa kwenye mfumo uliyopo ndani ya saa kumi na mbili kabla ya muda wa safari.

(2) Tozo itatozwa kwa kila amri ya kufuta au kurekebisha amri ya awali na malipo hayo yatalipwa kabla ya amri hiyo kuwasilishwa kwa Mamlaka.

Uwajibikaji unaotokana na

50. Mamlaka haitawajibika kwa ucheleweshaji wowote wa usafirishaji au kutosafirisha shehena kutokana

ucheleweshaji wa usafirishaji wa bidhaa

na wasafirishaji au mawakala wao kushindwa kuzingatia kanuni zinazotumika katika usafirishaji wa bidhaa hizo katika bandari yoyote.

Upimaji wa uzito

51.-(1) Endapo uzito au kipimo cha ujazo wa bidhaa hakipo, bidhaa zitapimwa uzito na Mamlaka na tozo zake zitalipwa na mtu ambaye atawasilisha nyaraka ya agizo la uwasilishaji wa bidhaa au nyaraka ya agizo la upakiaji bidhaa kuhusiana na bidhaa hizo.

(2) Kifurushi chenye uzito wa kilo 1,000 au zaidi kitakuwa na uzito halisi ambao umeandikwa nje ya kifurushi karibu na alama ya chombo.

(3) Endapo kifurushi hakina alama, kitapimwa na Mamlaka na gharama zote za upimaji, uhudumiaji wa ziada, usafiri kutoka kwenye mzani wa kupimia uzito zitatozwa na kulipwa na mpokea shehena.

(4) Mamlaka haitawajibika kwa makosa yoyote katika uzito uliopatikana chini ya masharti ya kanuni hii.

Uwekaji wa alama kwenye vifurushi

52.-(1) Endapo bidhaa zimewekewa alama isiojitosheleza au zimewekewa alama kimakosa, Mamlaka, bila kujali kwamba ada na tozo zote zimetolewa au kulipwa, itamtaka mtu anayedai bidhaa hizo kuwasilisha kibali maalumu cha kutoa bidhaa hizo kilichosainiwa na wakala wa chombo, au fidia dhidi ya hasara au uharibifu wowote ambao Mamlaka itaupata kutokana na kuwasilisha shehena hizo kwa mtu huyo.

(2) Tozo ya kawaida itatozwa kwa shehena yote iliyobaki kwenye eneo la bandari kutokana na uwekaji alama usiojitosheleza au wenye makosa.

(3) Mamlaka haitawajibika kwa uharibifu wowote, upotevu, ucheleweshaji, au kutowasilishwa kwa shehena kunakosababishwa na uwekaji alama usiojitosheleza au wenye makosa.

Upelekaji wa bidhaa kwenye ghala la forodha

53. Uwasilishaji wa shehena kwenye idara ya forodha utahesabika kuwa ni uwasilishaji wa shehena hizo kwa mpokea shehena na Mamlaka haitawajibika kuhusiana na shehena baada ya kuwasilishwa.

Vifurushi vyenye

54.-(1) Endapo bidhaa zimeshushwa katika

kasoro

vifurushi vyenye dosari au vinavyovuja, bila kujali masharti ya kanuni ya 56 au hali ya kwamba Mamlaka imetoa stakabadhi kwa ajili ya bidhaa hizo, uwasilishaji wa shehena hautachukuliwa kuwa umefanywa kwa Mamlaka mpaka hapo vifurushi hivyo vitakapofungwa upya, kuwekwa beji, au kukarabatiwa katika hali nzuri na shehena hizo kukaguliwa mbele ya wakala wa chombo, na Mamlaka itachukuliwa kuwa imekubali kukabidhiwa kwa shehena hiyo zikiwa katika hali kama zilivyoonekana kwenye ukaguzi huo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kukataa kupokea bidhaa ambazo zimeletwa kwenye vifurushi vyenye dosari au vilivyo katika hali ya kuvuja hadi pale vifurushi hivyo vitakaporekebishwa vizuri au bidhaa kuwekwa kwenye mifuko mipya au vifurushi vimerekebishwa vizuri kwa kiwango cha kuiridhisha Mamlaka.

Ufunguaji wa shehena

55.-(1) Bidhaa hazitafunguliwa ndani ya bandari bila kibali maalumu na usimamizi wa Mamlaka na makapi au vitu vingine vinavyotokana na bidhaa zilizofunguliwa vitafagiliwa na kuondolewa na mmiliki au wakala wa bidhaa hizo.

(2) Bidhaa zinaweza kuondolewa na Mamlaka kwa gharama za mmiliki au wakala huyo.

Tindikali na dutu zinazofanana na tindikali zilizoletwa katika hali ya kuvuja

56.-(1) Endapo tindikali, grisi, mafuta, lami,rangi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo ambavyo vinawasilishwa kwa Mamlaka vikiwa katika hali ya kuvuja, Mamlaka inaweza-

(a) kurekebisha kifurushi kinachovuja au chenye dosari na iwapo kuna umwagikaji uliosababishwa na kifurushi kuvuja au kuwa na dosari, utasafishwa na uharibifu uliotokea utarekebishwa kwa gharama ya mmiliki, na

(b) kujaza tena kifurushi ambacho vitu vilivyokuwemo awali vilivuja kwa kuweka vitu vinavyofanana na hivyo kutoka kwenye vifurushi vingine vinavyovuja au kuharibiwa ambavyo ni sehemu ya shehena hiyo kwa gharama ya mmiliki.

(2) Endapo kifurushi kimerekebishwa au kujazwa tena, mpokea shehena au mmiliki hatakuwa na madai dhidi ya Mamlaka kwa hasara au uharibifu unaotokana na marekesbisho, ukarabati au ujazwaji mpya wa kifurushi hicho:

Isipokuwa kwamba, mmiliki anaweza, wakati wa kuwasilisha agizo lake la usafirishaji kuitaarifu Mamlaka kwamba anataka vitu hivyo viwekwe pembeni, na kwa hali hiyo vinaweza kuondolewa na kuwekwa sehemu ya kuhifadhia au kuwekwa kwenye ghala kwa gharama zake.

Tozo kulipwa kabla au kuwekewa dhamana

57. Ada na tozo zinazolipwa kwa Mamlaka kwa ajili ya bidhaa zote zilizoshushwa, kuhamishwa au kuhifadhiwa ghalani zitalipwa, au dhamana toshelevu itatolewa kwa ajili ya malipo hayo, kabla ya maagizo ya kutolewa au kupelekwa kwaajili ya kufanyiwa kazi, na Mamlaka itazuia kuondolewa kwa shehena yoyote kutoka katika maeneo yake endapo ada au tozo zozote zinazotakiwa kulipwa na Mpokea shehena hazijalipwa.

## SEHEMU YA SITA
## UHUDUMIAJI WA BIDHAA HATARISHI

Notisi ya bidhaa hatarishi iliyopo ndani ya chombo

58.-(1) Nahodha au wakala wa chombo kilichobeba bidhaa hatarishi kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi, ndani ya saa arobaini na nane kabla ya kuwasili atatakiwa kutoa notisi ya bidhaa hatarishi kwa Mamlaka na bidhaa hizo hazitapakuliwa kabla ya nyaraka za usalama wa bidhaa hazijawasilishwa kwa Mamlaka.

(2) Nyaraka ya taarifa za usalama wa mizigo itajumuisha-

(a) jina sahihi la kitaalamu;
(b) uzito;
(c) namba ya Umoja wa Mataifa kama ipo;
(d) daraja katika Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi kwa kila shehena;
(e) tahadhari ya uhudumiaji, usalama na kiafya;
(f) hatari inayotokana na shehena husika;
(g) taratibu za dharura; na
(h) aina ya vifungashio.

Upakiaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi au zinazoweza kulipuka

59.-(1) Bidhaa hatarishi kama ilivyoainishwa katka Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi hazitapakiwa kwenye chombo bila kibali kutoka kwa Mamlaka.

(2) Mamlaka katika kutoa kibali, kwa mujibu wa kanuni hii, itahakikisha kwamba upakiaji na uhifadhi unafanyika kwa mujibu wa masharti ya usalama yaliyoainishwa na Mamlaka au na sheria nyingine inayohusika.

Maelekezo ya Mamlaka juu ya bidhaa hatarishi

60. Mamlaka, kwa maslahi ya usalama, ulinzi, utaratibu mzuri na uhifadhi wa mazingira na kwa gharama ya mmiliki au nahodha wa chombo inaweza-

(a) kuidhinisha upakuaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi katika maeneo yaliyotengwa ndani ya bandari kwa kuzingatia taratibu za uhudumiaji na uhifadhi wa shehena hatarishi zilizowekwa na Mamlaka au sheria nyingine yoyote inayohusika;

(b) kuamuru shehena hatarishi kupakuliwa kutoka kwenye chombo, kuondolewa bandarini au kushughulikiwa vinginevyo;

(c) kuamuru kwamba bidhaa hatarishi zizuiliwe au kurejeshwa ndani ya chombo ambacho kilipakua, ziharibiwe, au zishughulikiwe kwa namna ambayo Mamlaka itaona inafaa kwa gharama ya mmiliki au nahodha wa chombo kilichopakua shehena hiyo;

(d) kuamuru kwamba vyombo vyenye shehena hatarishi ndani yake ambavyo vimefungwa katika gati vina wafanyakazi na vifaa vya kutosha vya kudhibiti moto;

(e) kuamuru kwamba nahodha wa chombo chenye bidhaa hatarishi achukue hatua za tahadhari kama Mamlaka itakavyoona inafaa; na

(f) kuruhusu kuondolewa kwa mizigo iliyoainishwa katika orodha ya mizigo:

Isipokuwa kwamba, Mamlaka inaweza kuruhusu kuondolewa kwa mzigo uliozidi baada ya kupata idhini ya mamlaka ya forodha.

Ufungaji na

61.-(1) Chombo kilichobeba au kinachotaka

uondoshaji wa chombo kilichobeba vilipuzi

kubeba, vilipuzi kitatia nanga au kuwekwa katika nafasi kiliyopewa na Mamlaka na hakitahamishwa kutoka kilipo bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mamlaka.

(2) Chombo kilichobeba vilipuzi kwa ajili ya kupakuliwa bandarini kinaweza, kwa utashi wa Mamlaka, kuletwa pembezoni mwa gati iliyoainishwa na Mamlaka na kupakua vilipuzi hivyo kwa haraka.

Ujazaji wa mafuta katika chombo kilichobeba vilipuzi

62. Chombo kilichobeba vilipuzi vilivyo kwenye vibebeo vilivyoidhinishwa na kinachohitaji kujaza mafuta kinaweza, kwa utashi wa Mamlaka, kuletwa pembezoni mwa gati iliyoainishwa na Mamlaka na ujazaji wa mafuta utafanyika kwa haraka.

Notisi ya upakiaji na upakuaji wa vilipuzi

63. Kabla ya vilipuzi kuhamishwa kutoka kwenye chombo chochote au kushushwa au kupakuliwa kutoka kwenye chombo chochote, itatolewa taarifa kwa Mamlaka kuitaarifu kuhusiana na aina na kiasi cha vilipuzi hivyo.

Masharti mbalimbali kuhusiana na uhudumiaji wa vilipuzi

64.-(1) Vilipuzi-

(a) havitapakuliwa, havitasafirishwa au havitahamishiwa kwenye chombo kingine isipokuwa kwa maelekezo na usimamizi wa Mamlaka;

(b) havitapakiwa, havitaletwa au havitawekwa ndani ya eneo la bandari tofauti na eneo ambalo limeteuliwa na Mamlaka;

(c) havitawekwa kwenye eneo la bandari mpaka pale chombo kitakapokuwa tayari kuvipokea.

(2) Gharama zinazotumika katika usimamizi, utoaji wa walinzi au miundombinu mingine kwa ajili ya uhudumiaji na upakuwaji wa vilipuzi, isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo katika Kanuni hizi, zitabebwa na mpokea shehena, msafirishaji wa shehena, au wakala, kwa kadri itakavyokuwa.

(3) Isipokuwa kwa ruhusa ya Mamlaka na kwa kuzingatia masharti ambayo Mamlaka inaweza kuweka, vilipuzi havitapakiwa au kupakuliwa au kuhudumiwa katika muda ulioruhusiwa.

(4) Kiasi cha vilipuzi vitakavyopitishwa na kuruhusiwa kushushwa kwa wakati mmoja vitadhibitiwa

na Mamlaka na kiasi hicho kinachodhibitiwa hakitazidishwa.

(5) Vilipuzi vitakavyosafirishwa, vitakavyopakiwa au vitakavyopakuliwa kutoka kwenye gari lolote kwenye njia za reli ndani ya eneo la bandari vitasafirishwa, kupakiwa na kupakuliwa kwa kuzingatia Kanuni hizi.

Ukaguzi na uchunguzi

65. Mtu anayesimamia vilipuzi au chombo au gari lenye vilipuzi, pale anapotakiwa na Mamlaka, ataonesha vilipuzi vyote vilivyo chini ya usimamizi wake au kwenye chombo chake na atatoa kila kifaa kinachofaa kuwezesha ukaguzi na uchunguzi wa vilipuzi hivyo ili kuhakikisha kama Kanuni hizi zimezingatiwa ipasavyo.

Utunzaji wa petroli na vimiminika vinavyoweza kuwaka

66. Kwa upande wa mafuta na vimiminika vingine vyote vinavyoweza kuwaka, Kanuni hizi zitatumika kama nyongeza ya na si kwa kukiuka sheria yoyote husika inayotumika.

Utunzaji wa kalisiamu ya *carbide*

67.Pamoja na mahitaji mengine chini ya Kanuni hizi, yafuatayo yatatumika katika utunzaji wa kalisiamu ya *carbide*:

(a) mmiliki wa chombo au nahodha atahakikisha kwamba kalisiamu ya carbide imewekwa katika chumba chenye hewa ya kutosha;

(b) kalisiamu ya carbide iliyoshushwa kutoka kwenye chombo itaondolewa bila ucheleweshaji na kupelekwa eneo lenye kibali cha uhifadhi au nje ya mipaka ya eneo la bandari;

(c) kalisiamu ya carbide haitaletwa au kushushwa ndani ya eneo la bandari isipokuwa kama itakuwa imefungwa kwenye vyombo vya chuma vilivyotengenezwa madhubuti au kulindwa ili visiweze kuvunjika au kuharibika au kukosa usalama;

(d) kasha lenye kalsiamu ya carbide halitafunguliwa ndani ya mipaka ya eneo la bandari isipokuwa katika sehemu yenye kibali cha kuhifadhi au kwa idhini ya maandishi kutoka kwa mamlaka husika, katika mahali patakapo elekezwa;

(e) mmiliki wa chombo, nahodha na mmiliki wa kalisiamu ya carbide pamoja na mtu yeyote anayehusika katika upakiaji na upakuaji watatakiwa kuchukua tahadhari stahiki ili kuzuia mlipuko; na

(f) mmiliki au nahodha wa chombo kilichobeba kalisiamu ya carbide, na mtu anayesimamia kalisiamu ya carbide, inapohitajika na Mamlaka ataonyesha kalisi ya carbide iliyopo ndani ya chombo au iliyo chini ya usimamizi wake au kwenye chombo chake na atatoa kila kifaa kinachofaa kuwezesha ukaguzi na uchunguzi wa kalisiamu ya carbide ili kuhakikisha endapo Kanuni hizi zimezingatiwa ipasavyo.

Uzingatiaji wa sheria na miongozo ya tasnia nyingine

68.-(1) Mtu anayejihusisha na vimiminika hatarishi na vinavyowaka atazingatia sheria nyingine pamoja na mikataba ya kimataifa inayohusiana na vimiminika hatarishi na vinavyoweza kuwaka au vilivyohifadhiwa katika makasha.

(2) Mtu anayehusika katika kuhudumia bidhaa hatarishi atazingatia viwango, taratibu, na mahitaji yaliyoainishwa katika Miongozo ya Tasnia ya Majini, ikijumuisha-

(a) Mwongozo wa Kimataifa wa Usalama kwa Meli za mafuta na Vituo vyake;

(b) Vigezo vya Msingi vya Vituo vya Majini na Maswali ya Tathmini;

(c) Kanuni za Uhudumiaji wa Gesi Kimiminika kwenye Meli na kwenye Vituo;

(d) Mwongozo wa Kufanya kazi kwa kuzingatia Kanuni za Usalama kwa Gesi ya Kimiminika cha Petroli na shehena za Gesi ya Kemikali Kimiminika; na

(e) Mwongozo wa Uhudumiaji, Uhifadhi, Ukaguzi na Uhakiki wa mipira ya kupakulia mafuta kwenye eneo la utekelezaji.

(3) Mamlaka inaweza kuruhusu chombo kufuata utaratibu au utaratibu tofauti na ule unaotakiwa na miongozo ya tasnia ya majini, iwapo itaridhika kwamba utaratibu tofauti ni salama kama inavyotakiwa na mamlaka

husika na ni kwa maslahi ya usalama, utaratibu mzuri, ulinzi wa mazingira na ufanisi wa kazi ya bandari.

Bidhaa hatarishi zilizoshushwa katika makasha ya ISO

69.-(1) Endapo bidhaa hatarishi zimehifadhiwa kwenye makasha ya ISO, wakala wa chombo atatoa tamko la ufungashaji kupitia mfumo uliopo kabla ya kasha kushushwa.

(2) Tamko la ufungashaji litaainisha-
(a) jina sahihi la kiufundi;
(b) uzito;
(c) namba ya Umoja wa Mataifa;
(d) daraja la kila shehena kwa mujibu wa Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi kwenye kasha; na
(e) tamko kuwa-
(i) kasha linafaa kusafirisha aina husika ya bidhaa hatarishi;
(ii) mizigo imehifadhiwa ipasavyo kwenye kasha; na
(iii) hakuna bidhaa nyingine ambayo haiendani na bidhaa hatarishi itawekwa kwenye kasha.

(3) Tamko la upakiaji litaambatana na kasha mpaka kituo cha mwisho.

(4) Endapo bidhaa hatarishi zinatakiwa kusafirishwa katika makasha ya ISO, kituo cha upakiaji kitatoa tamko la ufungashaji kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2) pamoja na kasha lililopakiwa.

(5) Tamko la ufungashaji litaambatana na kasha wakati wote na litatolewa kwa mmiliki au nahodha wakati kasha linapakiwa kwenye chombo.

(6) Makasha ya ISO yenye nembo ya Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi yatachukuliwa kana kwamba yana bidhaa hatarishi.

Makosa chini ya Sehemu ya Sita

70.-(1) Mtu anayekiuka masharti yoyote ya chini ya Sehemu hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi Dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania.

(2) Pamoja na adhabu zilizoainishwa chini ya

kanuni ndogo ya (1) upande uliokiuka utawajibika kufidia kiwango cha uharibifu uliotokea.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni hii, Mamlaka inaweza kuamuru kuondolewa kwa chombo kilichokiuka masharti kutoka kwenye gati na kupelekwa sehemu iliyoelekezwa na Mamlaka kwa gharama za mmiliki.

## SEHEMU YA SABA
## SHEHENA YA VIMIMINIKA VINAVYOWEZA KUWAKA

Matumizi ya Sehemu hii

71. Sehemu hii itatumika ndani ya eneo maalumu lililotengwa na kuzuiliwa kwa ajili ya kituo cha mafuta na kwa vyombo vinavyobeba vimiminika vinavyoweza kuwaka ndani ya mipaka ya bandari, na kwa vyombo vingine vyote au chombo kilicho karibu na miundombinu ya vituo vyote vya mafuta ndani ya bandari.

Vyeti vya bima na ukaguzi

72.-(1) Meli inayoingia kwenye mipaka ya bandari ikiwa imebeba vimiminika vinavyoweza kuwaka, itakuwa na cheti halali cha bima ya uchafuzi wa mazingira na cheti halali cha uchunguzi kilichotolewa nchi ya usajili wa meli au mamlaka inayotambuliwa na nchi ya usajili wa meli, kwa ajili ya kubeba vimiminika vinavyoweza kuwaka kama itakavyothibitishwa na Mamlaka.

(2) Mamlaka haitaruhusu chombo ambacho hakina vyeti vilivyorejewa katika kanuni ndogo ya (1), kuingia Bandarini.

Hali ya chombo

73.-(1) Chombo kitafungwa ipasavyo kwa madhumuni ya kukabiliana na hali yoyote ambayo inaweza kuathiri usalama, utaratibu, ufanisi na ufanyaji kazi wa bandari.

(2) Waya wa dharura unatakiwa uandaliwe na kutunzwa muda wote kwa kipindi chote ambapo chombo kipo bandarini, ili kurahisisha chombo cha kuvuta meli kiweze kufunga na kuvuta wakati kitakapopata dharura ya moto Bandarini.

(3) Chombo kitakuwa na wafanyakazi wa kutosha, kwa madhumuni ya kukabiliana na hali yoyote ambayo inaweza kuathiri usalama, utaratibu, ufanisi na ufanyaji kazi wa bandari.

(4) Mifumo ya uingizaji au upozaji hewa, pale inapowezekana, itarekebishwa ili kuzuia kuingia kwa mvuke wa petroli.

(5) Mifuniko ya kuzuia mafuta yasimwagike baharini inatakiwa ifungwe kwa namna inayoridhisha.

(6) Kifuniko cha tangi lolote kitafunguliwa tu baada ya kuthibitishwa kuwa tangi hilo halina gesi.

(7) Chombo ambacho hubeba kimiminika kinachoweza kuwaka hakitazidi umri wa miaka kumi na tano isipokuwa kimeidhinishwa na mamlaka husika.

Uondoaji wa chombo

74. Endapo Mamlaka itaona ni muhimu au kwa maslahi ya usalama, utaratibu, ufanisi na utendaji kazi wa bandari, inaweza kuamuru kuondolewa kwa chombo chenye kimiminika kinachoweza kuwaka, kutoka kwenye gati ilipofunga, na nahodha wa chombo au mmiliki kuwajibika kwa gharama zilizohusiana na uondoaji huo.

Usalama wa tanki la mafuta

75.-(1) Mara tu baada ya vimiminika vyote vinavyoweza kuwaka kuondolewa katika meli ya mafuta, tangi za meli hiyo zitafungwa.

(2) Meli ya mafuta haitakaa ndani ya mita thelathini kutoka kwa chombo kingine chochote isipokuwa kwa maelekezo ya Mamlaka.

kufungwa kwa mlango wa sitaha ya shehena

76. Wakati ambapo shehena inashughulikiwa au kuingizwa kwenye chombo, milango yote ya sitaha ya mizigo na milango yote ya sitaha inayoelekea kwenye sitaha ya mizigo itafungwa, na milango hiyo inaweza tu kufunguliwa kwa madhumuni ya kuingia na kutoka pale ambapo ni muhimu kwa utendaji kazi wa chombo.

Upakuaji wa gesi

77-(1) Meli ya mafuta inaweza, kwa kibali cha maandishi cha Mamlaka na kwa kuzingatia masharti ambayo Mamlaka inaweza kuweka kwa maslahi ya usalama, utaratibu, ufanisi na utendaji kazi wa bandari, kupakua gesi bandarini.

(2) Maombi ya kupata kibali cha kupakua gesi bandarini kwa Mamlaka yataambatishwa na taarifa iliyosainiwa na nahodha inayothibitisha kwamba kuna mitambo inafaa na ina ufanisi katika upakuaji wa gesi

ndani ya chombo.

(3) Endapo msukumo unapoongezeka kwenye tanki lolote kutokana na mgandamizo wa hewa au njia nyinginezo, kabla ya kuanza zoezi la upakuaji, nahodha atathibitisha kuwa vali zote za njia ya gesi ziko katika utaratibu wa kufanya kazi.

(4) Kifuniko cha tangi lolote kitafunguliwa tu baada ya kuthibitishwa kuwa tangi hilo halina gesi.

(5) Endapo upakuaji wa gesi unaruhusiwa kabla ya kuendelea na upakuaji, matanki yote yatafungwa kikamilifu kwa usalama kabla ya kuanza upakuaji.

Kufungwa kwa vali gawanyishi

78. Vali za chombo na vali za bomba la upokeaji zitafungwa hadi pale ambapo-

(a) muunganisho wa bomba umefanywa;
(b) vali za mizigo za meli zimewekwa na vali za kutolea nje zimekaguliwa;
(c) tahadhari zote za usalama zimezingatiwa; na
(d) ruhusa ya kuanza kusukuma imetolewa na Mamlaka.

Masharti ya kupampu

79.-(1) Mara tu baada ya kuanza kupampu, na wakati msukumo kamili umefikiwa, nahodha atahakikisha kwamba hakuna mafuta au maji ya farumi yanayomwagwa baharini.

(2) kupampu vimiminika vinavyoweza kuwaka na uwekaji wa farumi utakoma kwa amri ya afisa aliyeidhinishwa na Mamlaka ambaye atamjulisha Nahodha Mkuu Bandari juu ya hatua yoyote iliyochukuliwa -

(a) wakati amri hiyo imetolewa kwa mujibu wa masharti mengine yoyote ya kanuni hii;
(b) ikiwa taa haziwaki ama kwenye sitaha ya mizigo au kwenye gati;
(c) karibu na dhoruba ya umeme na hadi hatari yote ipite;
(d) endapo kutatokea tukio sio la kawaida la mvuke kwenye chumba cha injini au pampu ; au
(e) endapo kutatokea tukio lolote na kwa ushauri ya Mamlaka haitokuwa salama kwa ufanyaji kazi wa chombo.

Uhudumiaji wa Vimiminika vinavyoweza kuwaka

80. Kabla ya kuanza kuhudumia shehena ya vimiminika vinavyoweza kuwaka, nahodha wa chombo atahakikisha kwamba-

(a) vali zote zinazomwaga maji baharini na katika vyumba vya pampu na sehemu inayotenganisha chumba cha injini na sehemu ya mizigo zinafungwa kwa uimara wakati wote wa upakuaji au shughuli ya chombo, isipokuwa vali hizo zinaweza kufunguliwa kwa lengo la kusafisha bomba za mafuta kwa kutumia maji na matundu ya kutolea maji melini yamefungwa kwa ufanisi;

(b) msukumo wakati wa kusukuma mafuta hufanyika kwa uangalifu na viungio vyote vya bomba vinavyoweza kuvujisha vimekaguliwa ili kupunguza hatari ya kumwagika; na

(c) chombo cha kukingia matone ya mafuta kinawekwa chini ya viunganishi vya mabomba ya aina mbalimbali.

Makosa chini ya Sehemu ya Saba

81. Mtu anayekiuka masharti yoyote chini ya Sehemu hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

## SEHEMU YA NANE
## UHUDUMIAJI WA VYOMBO VYENYE MAKASHA

Vyombo vyenye makasha kutumia gati maalumu

82. Nahodha wa chombo cha kubeba makasha atahakikisha kuwa chombo hicho kinapakua au kupakia mizigo kwenye kituo maalumu cha makasha au gati yoyote kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.

Usalama wa winchi ya kubeba makasha kwenye gati

83. Chombo hakitaegeshwa kwenye kituo maalumu cha makasha ikiwa winchi za kuhudumia makasha zimeshushwa chini au ikiwa winchi za kubebea makasha zimeegeshwa katika sehemu hatarishi za gati.

Wajibu wa nahodha

84.-(1)Nahodha atahakikisha kuwa-

(a) winchi za chombo zinawekwa kwenye sehemu

katika uhudumiaji wa makasha

yake hadi pale chombo kitakapokuwa kimeegeshwa kwa usalama kwenye gati;

(b) iwapo winchi zinazotumika kupakia au kupakua makasha ni za Mamlaka, winchi hizo zinawekwa katika nafasi ambayo hazitaathiri shughuli za upakiaji na upakuaji;

(c) vishikizi vya makasha yote vilivyowekwa kwenye sitaha vinafunguliwa baada ya chombo kufungwa kwa usalama na kabla ya muda uliowekwa kwa ajili ya kuanza upakiaji au upakuaji.

(2) Nahodha ataweka-

(a) namna salama ya kuyafikia makasha yote yaliyowekwa kwenye sitaha kwa ajili ya kuyafunga au kuyafungua;

(b) fimbo ya kutolea vishikizi vya makasha au kifaa kinachofanana na hicho chenye urefu wa kufikia vishikizi vyote kutoka juu ya sitaha.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (2) "namna salama" maana yake ni ngazi yenye urefu wa kutosha kufika juu ya daraja la juu zaidi la makasha lililoidhinishwa kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Makasha Salama wa mwaka 1972".

Vitendea kazi vya chombo kuwekwa tayari

85.- (1) Chombo kitakuwa na vifaa vya kuhudumia shehena vilivyo tayari baada ya chombo kufungwa kwa usalama katika gati kabla ya muda uliowekwa kwa ajili ya kuanza kwa shughuli za upakiaji au upakuaji.

(2) Matumizi ya winchi ya bandari yatategemea utashi wa Mamlaka.

Ufunguaji na ufungaji wa falka ya chombo kisicho na winchi

86. chombo ambacho hakina winchi ya kuhudumia mizigo na kinachohitaji winchi za bandari kufungua falka, mifuniko ya falka itatakiwa kuwa tayari kwa ajili ya kufunguliwa kabla ya muda uliopangwa kuanza shughuli za upakiaji au upakuaji.

Kasha kuwekwa alama

87.-(1) Kasha linaloshushwa litawekewa alama na namba kwa viwango vya ISO isipokuwa kwa makasha yanayomilikiwa na chombo ambapo alama nyingine toshelevu zitatumika

(2) Mamlaka haitawajibika kwa upotevu au kutokufikishwa kwa makasha ambayo hayana alama toshelevu.

Nahodha au wakala wa chombo kuwasilisha orodha ya shehena

88. Nahodha wa chombo au wakala wa chombo atalazimika, angalau saa ishirini na nne kabla ya chombo kuwasili au kuanza kazi kwa chombo bandarini, kuwasilisha orodha ya mizigo kupitia mfumo uliopo na itaonesha vitu vifuatavyo-

(a) nambari ya kasha;
(b) bandari ya kupakia;
(c) bandari ya kupakua;
(d) uzito wa jumla;
(e) hati ya mizigo majini au stakabadhi;
(f) jina la wakala wa mizigo, anwani na taarifa za mawasiliano;
(g) mmiliki wa kasha;
(h) taarifa za msafirishaji;
(i) majina ya mpokeaji na mtumaji shehena, anwani na taarifa za mawasiliano;
(j) maelezo ya makasha yenye vipimo nje ya viwango vya kawaida;
(k) taarifa ya makasha yenye jokofu na kiwango cha joto stahiki;
(l) taarifa za mizigo hatarishi kwenye makasha, kwa kutumia mfumo wa Shirika la Bahari Duniani wa kuorodhesha madaraja kulingana na Kanuni za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi;
(m) hali ya kasha kama vile kujaa, tupu, ghala kwa ghala, bandari kwa bandari, bandari kwa ghala, ghala kwa bandari;
(n) aina ya kasha;
(o) namba na maelezo ya vifurushi au bidhaa; na
(p) maelezo ya mzigo kichele ndani ya chombo.

Lakiri ya forodha iliyoidhinishwa

89.-(1) Kasha lenye uwezo wa kuwekwa lakiri litawekwa lakiri ya forodha iliyoidhinishwa itakayobandikwa katika sehemu ya kufungia kasha.

(2) Mamlaka haitawajibika kwa upotevu wa vitu vyovyote vilivyomo ndani ya kasha ikiwa halijawekewa lakiri au lakiri yake imeharibiwa kama inavyothibitishwa

na kumbukumbu zilizopo.

Kupakua kasha kwa ajili ya urahisi wa chombo

90.-(1) Chombo kinachotaka kupakua kasha lolote kwa ajili ya urahisi wake kwa nia ya kulirejesha kasha hilo ndani ya chombo kabla ya kuondoka, kitatakiwa kupata ruhusa ya Mamlaka kwanza.

(2) Mamlaka haitawajibika kwa hasara au uharibifu wa kasha lolote au vitu vilivyomo ndani ya kasha hilo.

(3) kasha ambalo halijapakiwa tena kabla ya chombo kuondoka litahifadhiwa hadi wakati ambao kasha hilo litakapoondolewa bandarini baada ya malipo ya tozo zinazohitajika kulipwa.

Mamlaka kuamua matumizi ya vitendea kazi vya chombo

91.-(1) Endapo mizigo mchanganyiko inatakiwa kupakuliwa kwenye kituo cha makasha, Mamlaka itakuwa na uhuru wa kutumia winchi za chombo au winchi za bandari zilizopo nchi kavu au winchi inayoelea.

(2) Nahodha atawajibika kwa ajili ya vifaa hivyo na atatozwa tozo kwa kiwango maalumu.

Kukabidhi au kupokea kasha

92.-(1) Utoaji au upokeaji kutoka kwenye gari utafanyika katika eneo la yadi ya makasha au eneo lingine lolote kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.

(2) Gari litatakiwa kuingia na kutoka katika kituo cha makasha kupitia lango la udhibiti na kufuata mfumo wa uongozaji wa magari ulioidhinishwa.

(3) Mamlaka haitawajibika kwa upotevu au uharibifu wa kasha lolote mara baada ya kukabidhiwa lakini itamuwajibisha msafirishaji kwa ubebaji wa kasha ndani ya kituo.

(4) Kwa kasha lililopokelewa kutoka kwenye gari, dhima ya Mamlaka itakoma baada ya kasha kupachikwa ipasavyo kwenye kifaa cha kunyanyulia shehena kwa ajili ya kusafirishwa.

Uhamishaji na ufunguaji wa makasha

93.-(1) Kwa utashi wa Mamlaka, kasha litahamishiwa sehemu iliyopangwa kutoka bandari hadi bandari na ghala hadi bandari kwa kutumia magari ya Mamlaka au usafiri utakaopangwa na Mamlaka.

(2) Maelekezo ya kufunguliwa kwa kasha yatatolewa na Mamlaka.

(3) Kasha la ghala hadi ghala litahamishiwa mahali palipotajwa katika hati ya shehena kwa gharama na hatari za mteja.

Kubadilisha hali ya kasha

94.-(1) Maombi ya mabadiliko ya hali ya makasha kutoka ghala kwenda ghala, ghala kwenda bandari au bandari kwenda bandari au kinyume chake yatawasilishwa kwa kupitia mfumo ulioidhinishwa na yatajumuisha-

(a) Hati za Shehena husika;

(b) namba za kasha; na

(c) hali ambayo mabadiliko yanaombwa.

(2) Endapo hadhi ya kasha haijatamkwa kwenye orodha ya shehena, kasha hilo litachukuliwa kuwa la bandari hadi bandari na kutozwa gharama za uhifadhi kwa mujibu wa Kitabu cha Tozo.

(3) Marekebisho ya hali ya kasha kutoka bandari hadi bandari, bandari hadi ghala na ghala hadi ghala au kinyume chake yatapokelewa kabla ya chombo kilichobeba kuanza kufanya kazi.

(4) Endapo ombi la marekebisho limepokelewa baada ya kasha kushushwa, tozo ya uhifadhi shehena itatozwa kwenye kasha na shehena hadi tarehe ya marekebisho.

(5) Endapo marekebisho yamepokelewa baada ya kasha kusafirishwa, gharama za upakiaji zitatozwa kupitia ankara ya Huduma ndogondogo za Bandari.

Ufungaji wa bidhaa usiofaa ndani ya makasha

95.-(1) Shehena zote zitapakiwa sawasawa na kufungwa vyema ndani ya kasha ili kuhakikisha uthabiti wa kasha.

(2) Makasha nusu na makasha kichanja yatafungwa na kukazwa vizuri na kupangwa kwa mujibu wa sheria husika.

(3) Msafirishaji na mpokeaji wa shehena atawajibika kwa ajali zozote zinazotokana na ufungaji wa mizigo usiofaa ndani ya kasha.

## SEHEMU YA TISA
## UHAMISHAJI, UEGESHAJI WA CHOMBO NA MASUALA YANAYOHUSIANA

Nahodha Mkuu wa Bandari kupanga na kusimamia gati

96.-(1) Chombo kitatumia gati iliyopangwa na Nahodha Mkuu wa Bandari na kinaweza kupelekwa kwenye gati lingine lolote kama atakavyoelekeza Nahodha Mkuu wa Bandari.

(2) Katika kupanga gati Nahodha Mkuu wa Bandari atazingatia-

(a) mahitaji ya kimkataba na mahitaji mengine ya waendeshaji wa vituo wanaofanya kazi kwenye gati hiyo;

(b) utaratibu mzuri na ufanisi wa kazi ya bandari; na

(c) mahitaji ya afisa anayehusika na upangaji wa ratiba ya vyombo.

(3) Nahodha Mkuu wa Bandari atakuwa na udhibiti na mamlaka ya kusimamia uegeshaji na ufungaji wa chombo kilichopokelewa kwenye gati binafsi.

(4) Chombo kinachoelekea kwenye gati, hakitakiwi kuegemea upande mmoja lakini kinatakiwa kititie kwa nyuma au kiwe na uwiano sawa.

(5) Nahodha Mkuu wa Bandari ataamua utaratibu wa utoaji wa shughuli za meli, ambazo ni pamoja na huduma za uongozaji wa meli, uvutaji na huduma ya uegeshaji na ufungaji wa vyombo bandarini .

(6) Nahodha Mkuu wa Bandari katika kuamua eneo la gati chini ya kanuni hii, atazingatia maslahi ya usalama, ulinzi na utaratibu mzuri, utendaji bora wa bandari na uhifadhi wa mazingira.

Notisi ya kuhamisha chombo bandarini

97.-(1) Nahodha hatahamisha chombo ndani ya bandari bila ya ruhusa ya Nahodha Mkuu wa Bandari.

(2) Ruhusa iliyorejelewa katika kanuni ndogo ya (1), itaombwa kwa Nahodha Mkuu wa Bandari angalau saa moja kabla uhamishaji wa chombo uliyokusudiwa.

Notisi ya ukarabati wa injini

98.-(1) Wakala au nahodha hatafanya ukarabati wa injini ya chombo bila kuwasilisha maombi kwa maandishi na kuruhusiwa na Nahodha Mkuu wa Bandari

(2) Wakala au nahodha anayekusudia kukarabati injini ya chombo bandarini atazingatia masharti yafuatayo katika kipindi cha ukarabati wa chombo:

(a) wakati chombo kikiwa nangani-

(i) kuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi ndani ya chombo wenye uwezo wa kugeuza kebo na kuweka ishara za nanga na kuchukua hatua zinazofaa endapo kutatokea dharura; na

(ii) inapotokea dharura, kumjulisha Nahodha Mkuu wa Bandari bila kuchelewa na kwa njia za moja kwa moja ikiwemo kutumia njia za mawasiliano za mikondo iliyoidhinishwa.

(b) chombo kikiwa kwenye gati-

(i) kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Nahodha Mkuu wa Bandari;

(ii) kuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi ndani ya chombo kwa ajili ya kuchukua hatua zinazotakiwa wakati wa dharura;

(iii) inapotokea dharura, kumjulisha Nahodha Mkuu wa Bandari bila kuchelewa na kwa njia za moja kwa moja ikiwa ni pamoja na matumizi ya Mkondo wa Mawimbi ya Mawasiliano ya Masafa Marefu 12 au 16; na

(iv) kuwekewa nyaya za kuvutia za dharura ubavuni, mbele na nyuma ya chombo.

(3). Endapo kuna dharura ndani ya chombo wakati wa ukarabati, Nahodha Mkuu wa Bandari anaweza kuelekeza chombo hicho kuhamishwa na kupelekwa mahali pengine.

(4) Endapo wakala au nahodha anashindwa kuhamisha chombo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) Nahodha Mkuu wa Bandari ataamuru utoaji wa boti ya kuvuta meli, uongozaji na genge la kufungua meli kwa ajili ya kuhamisha chombo kinachokarabatiwa na gharama zote zitakazotumika zitalipwa na wakala au nahodha.

(5) Mamlaka inaweza, kwa madhumuni ya usalama,

ulinzi, utaratibu na utendaji bora wa bandari, au uhifadhi wa mazingira, kukitaka chombo kuhama kutoka kwenye gati kwenda sehemu nyingine ya bandari.

(6) Gharama za uhamishaji uliorejewa katika kanuni ndogo ya (5) zitalipwa na nahodha isipokuwa kama imekubaliwa vinginevyo.

Taa za chombo

99. Chombo kilicho njiani au kilichotia nanga kitawashwa taa zinazotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Kimataifa za Kuzuia Kugongana kwa Vyombo Baharini za mwaka1972 kati ya masaa ya machweo na mawio.

Ukodishaji wa stima ya kuvuta chombo

100. Mamlaka, kwa kuzingatia masharti yafuatayo, itatoa huduma ya kuvuta meli na vifaa vingine vya kuvutia-

(a) wakati wa ukodishwaji wa stima ya kuvuta meli, nahodha na wafanyakazi wa chombo watakuwa watumishi, watatambuliwa na watakuwa chini ya usimamizi wa mkodishiwa au watumishi wake au wakala, na mtu yeyote aliye ndani ya chombo kilichokodishwa ambaye anaweza kuajiriwa au kulipwa na Mamlaka atachukuliwa kuwa mtumishi wa mkodishiwa;

(b) Mamlaka haitawajibika kwa uharibifu wowote uliofanywa na au kwenye tagi ya kuvutia meli, au uliofanywa na au kwenye chombo kilichokodiwa, au kwa majeraha yoyote kwa mtu binafsi au kupoteza maisha, kutokana na sababu yoyote, ikiwa ni pamoja na uzembe wa watumishi au mawakala wa Mamlaka, kutokuwa kwenye hali ya usalama majini, kutofaa au kuharibika kwa stima ya kuvutia meli, mitambo yake, boila, vifaa vya kuvutia, vifaa au tundu la nanga, ukosefu wa hifadhi ya mafuta au mwendokasi;

(c) mkodishwaji atalipa hasara au uharibifu na majeraha au kupoteza maisha na pia ataifidia Mamlaka dhidi ya madhara yote iliyopata:

Isipokuwa kwamba, dhima yoyote kwa ajili ya hasara au uharibifu kama ilivyoainishwa hapa haisababishwi na ukosefu wa uangalifu wa Mamlaka katika kuziweka tagi zake za kuvutia meli katika hali ya usalama

majini kwa ajili ya urambazaji wakati wa kutoa huduma ya uvutaji meli na huduma nyingine, na wajibu wa kuthibitisha kushindwa kwa Mamlaka kuwa na uangalizi huo utakuwa juu ya mmiliki wa chombo cha kuvuta; na

(d) kwa madhumuni ya kanuni hii "wakati wa kuvuta" utajumuisha kipindi kinachoanzia wakati ambao tagi ya kuvuta chombo iko kwenye hali ya kupokea maagizo ya moja kwa moja kutoka kwa chombo cha mkodishiwa ili kuchukua kamba au waya ya kuvutia imefikishwa kwenye boti ya kuvutia chombo, chochote kitakachotokea mapema zaidi, na kukamilika wakati maagizo ya mwisho kutoka kwa chombo cha kukodisha ya kutupa kamba au waya yametekelezwa, au kamba imetolewa na boti ya kuvutia chombo iko salama au chombo kiko salama, chochote kitakachotokea mwisho.

Notisi ya chombo kuondoka

101.-(1) Nahodha wa chombo, kabla ya chombo kuondoka, atatoa taarifa kwa Mamlaka akiainisha muda ambao chombo kitaondoka bandarini na notisi hiyo itathibitishwa na Nahodha Mkuu wa Bandari.

(2) Mamlaka itatoa ruhusa ya kuondoka bandarini kwa kutoa kibali kwa chombo kuondoka bandarini kupitia mfumo uliopo.

(3) Kabla ya chombo kuondoka bandarini, mmiliki, nahodha au wakala wa chombo atawasilisha kwa Mamlaka, na inapohitajika kwa mwendesha kituo, orodha ya abiria na wafanyakazi.

Nanga kuwa tayari kutoswa

102.-(1)Chombo kinachoingia au kutoka bandarini kitakuwa na nanga na nyaya zikiwa wazi na tayari kwa ajili ya kutumika.

(2) Endapo nanga, au mnyororo au waya wa chombo umeachia, umeteleza au kupotea ndani ya bandari, nahodha atatoa taarifa kwa Mamlaka mahali ilipo nanga, mnyororo au waya.

(3) Mamlaka inaweza kuamuru kwamba nanga, mnyororo au waya uliorejewa katika kanuni ndogo ya (2) urejeshwe kwa gharama ya mmiliki au wakala wa chombo.

Kutoa taarifa ya uharibifu

103.Nahodha au wakala wa chombo kilichoharibu mali yoyote ndani ya bandari, ikiwa ni pamoja na kuchafua au kuhamisha boya, kifaa cha usaidizi wa ungozaji au njia ya uongozaji-

(a) atatoa taarifa mara moja kwa Mamlaka na mamlaka nyingine zinazohusika;

(b) atawasilisha kwa Mamlaka taarifa kamili ya maandishi inayoainisha mazingira ya tukio, ndani ya saa ishirini na nne baada ya tukio au kabla ya meli kuondoka bandarini, chochote kitakacho tangulia; na

(c) atatoa maelezo yoyote ya ziada ambayo Mamlaka inaweza kuhitaji.

## SEHEMU YA KUMI
## VYOMBO VIDOGO, VYA ASILI NA VYA BURUDANI

Leseni ya uendeshaji na utiaji nanga wa chombo kidogo, cha asili au cha burudani

104.-(1) Chombo kidogo, cha asili au cha burudani hakitaendeshwa au kuegeshwa bandarini bila kuwa na leseni ya boti iliyotolewa na mamlaka husika kwa malipo ya ada kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

(2) Chombo kidogo kitasajiliwa na mamlaka husika.

(3) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) hayatatumika kwa stima ya kuvuta meli, tishari, boti yenye injini, mtumbwi au chombo chochote kidogo kinachomilikiwa na Mamlaka au Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(4) Vyombo vidogo, vya asili na vya burudani vitatia nanga kwa ajili ya kukaguliwa na kupewa ruhusa katika sehemu iliyoidhinishwa na Mamlaka na vitaacha njia wazi mbali na vyombo vingine.

Kuweka au kuendesha chombo kidogo, cha asili au cha burudani

105. Chombo kidogo, cha asili na chombo cha burudani kitaegeshwa tu au kuendeshwa bandarini kwa ruhusa ya Nahodha Mkuu wa Bandari ambaye anaweza kuonyesha mahali kinapoweza kuegeshwa au kuendeshwa.

Ufungaji wa chombo kidogo, cha asili au cha

106.-(1) Chombo kidogo, cha asili na cha burudani, hakitafungwa kwenye gati, nguzo, rundo au boya la Mamlaka isipokuwa kwa idhini ya Mamlaka.

burudani katika gati

(2) Chombo kidogo, cha asili na cha burudani hakitaegeshwa kando ya sehemu yoyote ya kushukia abiria au ngazi ya kupandia chomboni yenye urefu kuliko inavyotakiwa kupandisha au kushusha abiria na mizigo yao, isipokuwa wakati wa kusubiri ili kutozuia njia kitaegeshwa katika umbali utakaoamuliwa na Nahodha Mkuu wa Bandari.

Ufungaji chombo chombo kidogo, cha asili au cha burudani kwa matengenezo

107. Chombo kidogo, chombo cha asili na burudani havitaletwa ufukweni kwa madhumuni ya ukarabati isipokuwa mahali palipoidhinishwa au mahali pengine popote patakapotengwa na Mamlaka kwa dhumuni hilo.

Abiria na mizigo kushushwa sehemu iliyopangwa

108.-(1) Boti au mashua inayoelekea au kuondoka kutoka pembezoni mwa meli, chombo kidogo, cha asili na cha burudani hakitapandisha au hakitashusha abiria au kupakia au kupakua mizigo isipokuwa katika sehemu iliyoteuliwa na Mamlaka.

Gati ya Rais

109. Boti haitafungwa kwenye Gati ya Rais ya Dar es Salaam au kutia nanga ndani ya umbali wa futi 100 kutoka hapo.

Nahodha wa chombo kidogo, cha asili au cha burudanikuw asilisha taarifa

110.-(1) Nahodha wa chombo kidogo, cha asili na cha burudani kinachowasili bandarini atatoa taarifa inayohusiana na usalama wa chombo hicho majini, mizigo na abiria kama wapo.

(2) Nahodha wa chombo kinachoingia bandarini anaweza kutakiwa kutoa cheti cha chombo chake.

Mali ambayo haina mmiliki iwasilishwe kwa Mamlaka

111. Mtu anayesimamia chombo chenye leseni ya kubeba abiria atawasilisha kwa Mamlaka mali iliyobaki katika chombo chake ikiwa hakuna mtu anayeidai.

Uwajibikaji juu ya upotevu au majeraha

112. Sehemu hii haitachukuliwa kuwa inaweka wajibu au jukumu lolote kwa Mamlaka kuhusiana na hasara au majeraha yaliyosababishwa na vitendo au uzembe wa mmiliki au mtu anayesimamia chombo chenye leseni.

Zuio kwa vyombo vidogo kupeleka vileo kwa wafanyakazi wa meli

113.-(1) Mmiliki wa chombo au mfanyakazi wa boti au mtu aliyeajiriwa na mmiliki huyo hatasambaza, hatasafirisha au hatapeleka kileo chochote kwenye meli yoyote iliyotia nanga au kufungwa bandarini, isipokuwa -

(a) vileo vinaweza kununuliwa kwa ridhaa ya nahodha kutoka kwa mtu aliyepewa leseni na Mamlaka kwa ajili ya kuendesha biashara hiyo ndani ya eneo la bandari; na

(b) vileo vinavyoweza kuondolewa kwa mujibu wa sheria na kanuni za forodha kutoka kwenye ghala kwa ajili ya kusafirishwa nje ya mipaka ya bandari au kwa ajili ya kuhifadhiwa ndani ya chombo.

(2) Mamlaka inaweza kusimamisha au kufuta leseni endapo mmiliki atakiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1).

Makosa chini ya Sehemu ya Kumi

114. Mmiliki au mtu anayesimamia chombo kidogo, chombo cha asili na chombo cha burudani ambacho kimekiuka masharti ya Sehemu hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua dola za Marekani mia mbili au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MASHARTI MAALUMU KUHUSIANA SHEHENA YA MAJAHAZI

Shehena ya jahazi kuhudumiwa katika maeneo yaliyoidhinishwa

115- (1) Shehena ya jahazi inaweza kupakiwa na kupakuliwa na Mamlaka ndani ya eneo la bandari kama ilivyopangwa na Mamlaka kwa gharama kama itakavyoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) na kwa kuzingatia matakwa ya udhibiti, Mamlaka inaweza kuruhusu mzigo wa jahazi kupakiwa au kupakuliwa na wafanyakazi wa mmiliki ndani ya eneo la bandari kama ilivyopangwa na Mamlaka, kwa gharama kama itakavyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Shehena ya jahazi inayoingia na kusafirishwa

116. Shehena inayoingia nchini au kusafirishwa nje ya nchi kutoka na kwenda kwenye jahazi inaweza, kwa utashi wa Mamlaka, kuhifadhiwa kwenye eneo la Mamlaka

nje ya nchi

katika sehemu zilizopangwa kwa ajili ya kuweka shehena ya jahazi na kwa tozo kama itakavyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Mamlaka kutowajibika kwa upotevu au uharibifu

117. Endapo bidhaa zinapakiwa, kupakuliwa au kuhifadhiwa chini ya masharti ya Sehemu hii, Mamlaka haitawajibika kuhusiana na upotevu, kutofikishwa au kuzuiliwa au uharibifu wa bidhaa hizo endapo hasara, uwasilishaji usio sahihi au kuzuiliwa, au uharibifu huo umesababishwa na vitendo vya mmiliki.

Samaki waliokaushwa na kuwekwa chumvi

118.-(1) Samaki waliokaushwa na kuwekwa chumvi waliohifadhiwa kwenye eneo la Mamlaka wataondolewa katika eneo hilo ndani ya muda wa siku tatu.

Isipokuwa kwamba, muda huo unaweza kuongezwa na Mamlaka iwapo bidhaa hizo zimeingizwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa mujibu wa masharti ya Sheria za Forodha.

(2) Endapo bidhaa hizo hazijaondolewa ndani ya muda huo, Mamlaka inaweza kuuza bidhaa hizo kwa mnada wa hadhara kwa mujibu wa masharti ya Sheria, na inaweza, kutokana na mapato ya mauzo hayo kukata kiasi chochote kinachopaswa kulipwa kwa Mamlaka na itawasilisha bakaa, kama ipo, kwa mtu anayeonekana kwa Mamlaka kustahili kupata bakaa hiyo.

Uondoshwaji au uuzaji wa bidhaa

119. Endapo bidhaa nyingine tofauti na samaki waliokaushwa na waliotiwa chumvi zimewekwa kwenye eneo la Mamlaka, Mamlaka inaweza kutoa notisi kwa mtu anayehusika kuondoa bidhaa hizo ndani ya muda utakaoainishwa kwenye notisi, na iwapo bidhaa hizo hazitaondolewa ndani ya muda ulioainishwa, Mamlaka inaweza kuziuza na kugawanya mapato ya mauzo hayo kwa kukata kiasi chochote kinachopaswa kulipwa kwa Mamlaka na kuwasilisha bakaa, kama ipo, kwa mtu anayeonekana kwa Mamlaka kustahili kupata bakaa hiyo.

Isipokuwa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi hazitauzwa mpaka zitakapokuwa zimeingizwa kwa mujibu wa masharti ya sheria za Forodha.

Ushughulikiaji au uhudumiaji wa shehena za jahazi

120.-(1) Shehena kutoka au kwenda kwenye jahazi haitashushwa au kusafirishwa kwenye vituo, gati au sehemu za Mamlaka ambazo kwa kawaida hutumiwa na chombo au tishari.

(2) Winchi zilizosimikwa bandarini hazitatumika kwa madhumuni ya kushusha au kubeba shehena za jahazi, isipokuwa kwa ruhusa ya Mamlaka na kwa kuzingatia ulipaji wa tozo za kawaida zilizoanishwa katika Kitabu cha Tozo utakaofanywa na Nahodha au mmiliki wa jahazi.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## UHIFADHI WA SHEHENA

Mamlaka inaweza kukataa kuhifadhi baadhi ya shehena

121. Mamlaka inaweza kukataa kupokea bidhaa zifuatazo kwa ajili ya kuzihifadhi -

(a) vitu vya urefu, wingi au uzito usio wa kawaida, au wingi usiokuwa wa kawaida kuwianisha uzito wake;
(b) vitu visivyofungashwa au vilivyofungashwa vibaya ;
(c) bidhaa hatarishi ambazo zinaweza kusababisha madhara au uharibifu kwa watu au mali;
(d) bidhaa ambazo zinaharibika haraka na ambazo kwa asili zinaweza kuharibika kwa wingi au uzito au kwa kasoro zilizofichika za asilia, zenye matatizo au zenye asili ya kuharibika haraka;
(e) mbao;
(f) vyuma chakavu;
(g) wanyama; na
(h) bidhaa nyingine zozote ambazo Mamlaka inaweza kuona inafaa kuziwekea.

Tozo ya kubadilisha njia ya upakiaji wa bidhaa

122. Endapo kuna mabadiliko ya hali kutoka uwasilishaji au upakiaji wa moja kwa moja kuwa uwasilishaji au upakiaji usio wa moja kwa moja tozo za uhudumiaji zitabadilishwa kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Tozo za uhifadhi wa

123. Tozo za uhifadhi zitatozwa kwa mizigo inayoingizwa inchini ambayo nyaraka zake hazijapokelewa

mizigo inayoingizwa nchini

na Mamlaka au tozo zake hazijalipwa au kuwekewa dhamana:

Isipokuwa kwamba shehena hizo zitakuwa kwenye kipindi cha msamaha kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Tozo za mizigo ambayo haijaondolewa katika ghala la Mamlaka

124.-(1) Shehena zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo hazijaondolewa kwenye ghala na maeneo ya uhudumiaji mizigo ya Mamlaka ndani ya muda ulioainishwa kwenye kitabu cha Tozo, zitatozwa tozo ya utunzaji kwa kipindi chochote kilichozidi muda wa msamaha ulioanishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

(2) Shehena zilizoingizwa kutoka nje ya nchi iliyoko kwenye eneo lolote la bandari na ambayo nyaraka zake zinazohitajika hazijawasilishwa kwa Mamlaka ndani ya muda ulioanishwa kwenye Kitabu cha Tozo, zinaweza kuhamishwa na Mamlaka, ndani ya eneo la kuhifadhia au kutoka eneo la kuhifadhia hadi eneo lingine lolote ndani ya eneo la bandari na shehena yoyote inayohamishwa itatozwa tozo ya uondoshaji shehena kama ilivyoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

Shehena iliyozuiliwa na Forodha au Polisi

125.-(1) Bidhaa iliyozuiliwa na Forodha kwa madhumuni ya uchunguzi inaweza, kwa utashi wa Mamlaka, kusamehewa gharama za uhifadhi kuanzia tarehe ambayo nyaraka yake imesimamishwa na Forodha hadi tarehe ya kukamilika kwa uchunguzi.

(2) Bidhaa iliyozuiliwa na polisi kama bidhaa au mali iliyopatikana, itatolewa na Mamlaka kwa saini ya afisa polisi na shehena hiyo itarejeshwa kwa Mamlaka baada ya kukamilika kwa upelelezi au taratibu za mahakama kwa ajili ya kushughulikiwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo:

Isipokuwa kwamba, ucheleweshaji wowote uliosababishwa na muagizaji au wakala katika kipindi cha kuwekwa kizuizini hautapewa faida ya uhifadhi wa bure wa shehena hiyo.

Tozo ya uhifadhi wa shehena inayopakiwa

126.-(1) Isipokuwa kama itakuwa imeelezwa vinginevyo, gharama za kuhifadhi shehena zitatozwa kwa shehena inayosafirishwa nje ya nchi na kuanzia tarehe ya

nje ya nchi

kupokelewa na Mamlaka katika eneo la bandari kwa shehena hiyo inayosafirishwa nje ya nchi hadi tarehe ya upakiaji.

(2) Muda wa kuhifadhi wa bure kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo utatolewa kwa mizigo inayosafirishwa nje ya nchi.

Shehena iliyokataliwa

127.-(1) Shehena iliyokataliwa na kuachwa katika eneo la bandari itatatozwa tozo ya uhifadhi na tozo nyingine kama ilivyoainishwa katika kitabu cha Tozo.

(2) Shehena itachukuliwa kuwa imekataliwa ikiwa imepokelewa bandarini kwa ajili ya kusafirishwa lakini haijapokelewa kwa ajili ya kubebwa na chombo kilichotajwa katika nyaraka ya agizo la upakiaji shehena.

Shehena inayosafirishwa nje ya nchi inaweza kuhamishwa

128. Shehena inayosafirishwa nje ya nchi ambayo inadaiwa tozo ya uhifadhi inaweza kuhamishwa na Mamlaka kwenda sehemu yoyote katika eneo la bandari au kuachwa ilipo.

Isipokuwa kwamba shehena hiyo itatozwa tozo za ziada kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Uondoaji wa shehena inayosafirishwa nje ya nchi

129.-(1) Endapo muuzaji au msafirishaji wa shehena nje ya nchi anataka kuhamisha mizigo yoyote inayosafirishwa nje ya nchi ambayo tayari ipo kwenye eneo la kuhifadhia mizigo kwa madhumuni tofauti na ya usafirishaji, Mamlaka itatoa wafanyakazi na vifaa vinavyohitajika kwa tozo iliyoainishwa katika Kitabu cha Tozo na matumizi ya wafanyakazi binafsi kwa madhumuni haya hayataruhusiwa.

(2) Endapo uondoaji wa mizigo inayosafirishwa nje ya nchi ni kutoka kwenye eneo la Mamlaka la kuhifadhia mizigo kwenda kwenye ghala binafsi, nyaraka za upakiaji mizigo zitawasilishwa si chini ya saa arobaini na nane kabla ya kuisha kwa muda wa kuhifadhi shehena bure wa shehena husika.

(3) Endapo muuzaji bidhaa nje ya nchi au msafirishaji atashindwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (2), bidhaa zitatozwa tozo za uhifadhi hadi tarehe ambayo shehena hizo zitakapopakiwa kama ilivyoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

Kukosekana kwa eneo la uhifadhi wa shehena

130.-(1) Endapo Mamlaka itatamka kuwa hakuna nafasi ya kuhifadhi bidhaa bandarini mmiliki au wakala wake hataruhusiwa kuingiza bidhaa ndani ya eneo la bandari kwa muda utakaoainishwa na Mamlaka.

(2) Mtu ambaye anakiuka masharti ya kanuni ndogo (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania.

Msamaha wa tozo za uhifadhi wa shehena

131.-(1) Mamlaka inaweza, baada ya maombi, kutoa msamaha wa tozo za uhifadhi wa shehena.

(2) Maombi ya msamaha yatashughulikiwa kwa mujibu wa sera ya msamaha ya Mamlaka.

Kubadilisha umiliki wa shehena

132.Taarifa ya mabadiliko yoyote ya umiliki wa shehena itawasilishwa kwa Mamlaka mara tu baada ya mabadiliko hayo kufanyika na, kama taarifa hiyo haitatolewa, mmiliki wa awali atawajibika kulipa tozo zote.

Tozo za uhifadhi wa shehena inayopakiwa kutoka meli moja kwenda nyingine na shehena iliyo zidi kiwango cha forodha

133.-(1) Gharama za kuhifadhi shehena zitatozwa kwa shehena yote iliyoshushwa katika bandari na inatarajiwa kusafirishwa tena kwa chombo au shehena ya ziada iliyoshushwa:

Isipokuwa kwamba muda wa bure wa kuhifadhi shehena utatolewa kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

(2) Wakati inaposubiri kusafirishwa tena, shehena inayosafirishwa kwenda kituo kingine haitatoka chini ya himaya ya Mamlaka au mwendeshaji wa bandari kavu na haitafanyiwa mabadiliko yoyote, vinginevyo tozo za kawaida za shehena inayoingizwa kutoka nje ya nchi na kusafirisha nje ya nchi zitatumika.

Mizigo ya abiria ambayo haijaondolewa

134. Mizigo ya abiria ambayo haijaondolewa kutoka eneo la uchunguzi wa Forodha bandarini ndani ya saa ishirini na nne baada ya kibali cha kuondolewa itaondolewa na kuwekwa kwenye ghala na kutozwa tozo za uhifadhi wa mizigo zilizoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Madai ya marejesho ya tozo zilizozidi

135.-(1) Madai ya marejesho ya tozo zilizozidi yatawasilishwa kwa Mamlaka kabla ya kuisha kwa muda wa miezi mitatu kutoka tarehe ya kutozwa ushuru au tozo nyingine na yataambatishwa na nyaraka kama Mamlaka itakavyohitaji.

(2) Madai ya marejesho ya ushuru na tozo za bandari zilizotozwa zaidi yatashughulikiwa kwa mujibu wa sera ya madai ya Mamlaka.

(3) Isipokuwa kama masharti ya kanuni ndogo ya (1) yamezingatiwa, Mamlaka haitawajibika kwa malipo ya ziada wala madai hayo hayatazingatiwa.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
UHIFADHI WA SHEHENA KATIKA GHALA

Uhifadhi wa shehena inayosafirishwa nje ya nchi

136. (1) Mamlaka inaweza kuhifadhi bandarini shehena inayosafirishwa nje ya nchi isipokuwa mifugo kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) nafasi inapatikana;
(b) bidhaa zilizokusudiwa kuhifadhiwa katika maghala ya bandari zitasafirishwa kulingana na aina ya bidhaa hizo; na
(c) watu ambao sio wafanyakazi wa bandari hawataruhusiwa kufanya kazi katika maghala ya bandari bila idhini ya Mamlaka.

(2) Mamlaka inaweza, katika mazingira maalum, kuondoa huduma ya kuhifadhi mizigo inayosafirishwa nje ya nchi.

Tozo maalumu

137. Endapo huduma inayohusiana na bidhaa iliyohifadhiwa kwenye ghala la bandari haijajumuishwa kwenye Kitabu cha Tozo, huduma hiyo itatozwa tozo maalumu itakayoamuliwa na Mamlaka.

Uhifadhi wa shehena hatarishi

138.-Mamlaka inaweza, kwa malipo, na kwa maombi ya maandishi, kwa kutugemea upatikanaji wa vifaa muhimu na mahitaji ya usalama, kupokea shehena hatarishi zilizoainishwa katika Kanuni ya Kimataifa za Bidhaa Hatarishi katika maghala ya bandari.

Ufungashaji

139.-(1) Shehena inayosafirishwa nje ya nchi

wa shehena zilizohifadhi wa ghalani

iliyohifadhiwa kwenye miundombinu ya bandari itafungashwa vizuri kwa ajili ya kusafirishwa.

(2) Uchambuzi na urekebishaji mwingine wa shehena katika ghala la bandari hautaruhusiwa bila kibali cha Mamlaka.

Utoaji wa taarifa ya shehena na ulipaji wa tozo ya uhifadhi

140. Shehena haitatolewa kwenye maghala ya bandari kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi au kuwasilishwa ndani ya nchi mpaka maelezo yote ikijumuisha thamani ya shehena hiyo inapohitajika, iwe imewasilishwa kwa Mamlaka na tozo ya uhifadhi wa shehena imelipwa au dhamana imewekwa.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## KANUNI ZA JUMLA ZA USALAMA

Matumizi ya kanuni za Usalama

141. Kanuni za usalama zilizojumuishwa katika Sehemu hii zitatumika katika shughuli za bandari ndani ya eneo la bandari.

Wajibu wa Nahodha wa chombo juu ya usalama wa chombo

142. Nahodha wa chombo kilicho ndani ya mipaka ya bandari anawajibika kuhakikisha usalama wa chombo wakati wote na hakuna kitu katika Kanuni hizi kinachoweza kutafsiriwa kumuondolea nahodha jukumu hili.

Tukio la moto

143.-(1) Endapo litatokea tukio la moto kwenye chombo nahodha atatoa taarifa au ishara moja kwa Mamlaka na atachukua hatua za kuzuia moto huo kama Mamlaka itakavyoelekeza.

(2) Nahodha atapandisha bendera ya N.C ya Kanuni za Kimataifa na wakati huohuo atapiga mlio mmoja mrefu wa honi na milio mingine mifupi mitatu itakayopigwa kwa honi kwa mfululizo wa haraka na bendera itabaki juu mpaka moto ndani ya chombo utakapozimwa.

(3) Mamlaka inaweza, endapo kutatokea mlipuko mkubwa wa moto, kuuondoa umma katika eneo lililo karibu na moto na inaweza kufunga eneo lote au sehemu yoyote ya eneo la bandari kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

(4) Mtu aliye katika eneo la bandari hatapuuza maagizo ya afisa wa zimamoto, afisa polisi au mtu mwingine aliyeidhinishwa au kuzuia au kuingilia kwa njia yoyote shughuli za uzimaji moto.

(5) Mamlaka inaweza, pale inapotoa huduma ya uzimaji wa moto iwe kwa ombi la mtu au la, kutoza tozo kwa ajili ya huduma hiyo ya uzimaji moto kwa kiwango kilichoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Kupanda au kushuka kwenye chombo

144. Mtu hataruhusiwa, isipokuwa kwa ruhusa ya Mamlaka, kupanda au kutoka kwenye chombo wakati chombo hicho kiko katika mwendo wala mtu yeyote hatatoka au kupanda kwenye chombo isipokuwa kwa kutumia ngazi ya chuma au ngazi ya Nahodha.

Kutokuacha vitendea kazi vya chombo bandarini

145. Nahodha hataacha vifaa vya kuhudumia shehena katika eneo la bandari isipokuwa kwa ruhusa ya Mamlaka.

Kutogeuza chombo kwa kutumia injini kikiwa kwenye boya

146. Nahodha hatageuza chombo kwa kutumia injini wakati chombo kikiwa kimefungwa kwenye boya.

Katazo la kuwasha moto

147. Mtu hataruhusiwa kuwasha moto au kuweka mwanga karibu na vifuniko au katika sehemu zilipohifadhiwa bidhaa hatarishi:

Isipokuwa kwamba kanuni hii-

(a) haitazuia matumizi ya ufungaji wa taa ya umeme au taa ya usalama iliyotengenezwa kwa namna iliyoidhinishwa na Mamlaka au taa ya kuendeshea chombo au ishara zilizowekwa ili kuzuia hatari; na

(b) haitatumika kwa moto ulioko kwenye chumba cha injini kama umewekwa kwa uangalifu hapo awali.

Ulevi

148. Mtu atakayekuwa katika hali ya ulevi wa pombe au dawa za kulevya hataruhusiwa kuingia katika eneo la bandari.

Vifaa vya kunyanyua mifuniko ya staha

149. Nahodha atahakikisha kuwa mifuniko yote ya mbele na ya nyuma na mifuniko inayotumika kufunika staha ina vifaa vinavyofaa kwa ajili ya kunyanyua mifuniko hiyo bila ulazima wa mtu kwenda juu ili kurekebisha vifaa hivyo.

Katazo la kuweka bidhaa kwenye njia

150. Mtu hataweka bidhaa kwenye gati kwa namna inayozuia njia inayoelekea kwenye miundombinu inayotumika kwa ajili ya kuingia kwenye chombo na ikiwa nafasi yoyote imeachwa pembezoni mwa gati itakuwa na upana wa angalau sentimita 91  au futi tatu na itakuwa wazi bila vizuizi vyovyote isipokuwa miundombinu iliyosimikwa, mitambo na vifaa vinavyotumika.

Ukaguzi na majaribio ya mitambo ya kunyanyulia shehena

151. Mamlaka itahakikisha kuwa mashine za kunyanyulia vitu zimefanyiwa majaribio na kuchunguzwa kabla ya kuanza kutumika kwa utaratibu uliowekwa na Mamlaka.

Mamlaka inaweza kuharibu au kushughulikia shehena kwa namna nyingine

152. Ikiwa kuna dharura, au kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa bandari au chombo kilichomo, Mamlaka inaweza, kwa kushauriana na mamlaka husika, pale itakapoonekana inafaa kufanya hivyo, kuteketeza au kuziondoa shehena bila fidia kwa mmiliki wa shehena na gharama za uondoaji huo zitalipwa na mpokeaji wa shehena, mmiliki au wakala wa shehena hizo.

Kibali cha kufanya kazi zinazohusiana na moto

153.-(1) Mtu hatafanya kazi za moto kwenye chombo au ufukweni ndani ya eneo la bandari bila kibali kutoka kwa Mamlaka.

(2) Mamlaka itakagua mahali ambapo kazi za moto zitafanyika kabla ya kutoa kibali.

(3) Mamlaka itaweka masharti juu ya utendaji wa kazi za moto na kutoza tozo kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Uondoshaji wa mabaki ya gari au chombo

154. Mtu hataondoa mabaki ya gari au chombo katika eneo la bandari bila ruhusa ya Mamlaka au kinyume cha masharti yoyote yanayoweza kuwekwa na Mamlaka.

Makosa chini

155. Mtu anayekiuka masharti yoyote chini ya

ya Sehemu ya Kumi na Nne

Sehemu hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## USALAMA NA AFYA MAHALA PA KAZI

Uzingatiaji wa taratibu na tahadhari za usalama

156. Mtu aliye ndani ya eneo la bandari -
(a) atachukua tahadhari stahiki kwa ajili ya usalama wake, usalama wa wengine na mali;
(b) ataheshimu alama za usalama na mabango yaliyowekwa ndani ya eneo la bandari;
(c) hataendesha gari au mtambo wenye ubovu;
(d) atasafisha mazingira ya bandari na kuweka taka katika sehemu ya kuhifadhia;
(e) atavaa vifaa vya kinga;
(f) hatatupa taka ndani ya eneo la bandari; na
(g) atazingatia kanuni zinazosimamia usalama na afya.

Uendeshaji wa magari bandarini

157.- (1) Mtu anayeendesha gari katika eneo la bandari -
(a) atahakikisha kuwa gari liko katika hali nzuri;
(b) atakuwa na leseni hai ya kuendesha gari;
(c) atazingatia sheria na alama za usalama barabarani ndani ya maeneo ya bandari;
(d) atazingatia mwendokasi usiozidi kilomita 20 kwa saa;
(e) atahakikisha magurudumu yote ya gari yapo katika hali nzuri;
(f) atatoa taarifa kwa Mamlaka haraka juu ya ajali yoyote inayotokea katika eneo la bandari;
(g) hataendesha gari akiwa kwenye hali ya ulevi;
(h) hataendesha gari huku akitumia simu ya mkononi;
(i) hataendesha gari akiwa amefunga kizuia sauti cha sikio au spika ya sikio;
(j) atakuwa na alama ya pembetatu na kifaa cha kuzimia moto kinachofaa; na
(k) hatasababisha kizuizi barabarani, reli au njia za

kupita ndani ya eneo la bandari na mazingira yake.

(2) Wamiliki wa malori na madereva watahakikisha kuwa-

(a) malori yana vishikizi vya kasha za kufunga na kasha lazima lifungwe wakati wote linapokuwa limepakiwa kwenye lori;

(b) mifumo ya taa ikijumuisha taa ya kiashiria na taa za breki ziko katika hali nzuri ya kufanya kazi;

(c) lori limewekewa kifaa cha kuzimia moto;

(d) lori au trela lililobeba shehena ya nafaka limefunikwa na turubai ili kuzuia uchafuzi wa hewa;

(e) lori au trela lililobeba nafaka linapaswa kufunikwa kwa kubana hewa ili kuzuia kumwagika kwa nafaka katika maeneo ya bandari;

(f) lori lililobeba mzigo usiofungwa liwe na tela za kichanja zenye vigingi vya wima au mikunjo ya chuma ili kuweka mabomba ya chuma au mbao mahali pake; na

(g) lori limewekewa viakisi mwanga vinavyofaa mbele na nyuma.

(3) Vifaa vyote vitakuwa na haki ya njia ndani ya eneo la uendeshaji.

Makosa chini ya Sehemu ya kumi na tano

158. Mtu anayekiuka masharti yoyote chini ya Sehemu hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## UHIFADHI WA MAZINGIRA

Katazo la utupaji wa vitu bandarini

159.-(1) Mtu hatatupa, hataacha, hatamwaga au hataweka au hataruhusu au hatasababisha kutupwa, kuachwa, kumwagwa au kuwekwa ndani ya bandari kitu

chochote, nyenzo au kimiminika ambacho kinaweza kusababisha kizuizi, hatari, uchafuzi wa mazingira au kero.

(2) Gharama na madai yanayoweza kuingiwa na Mamlaka katika kuondoa kitu chochote au kimiminika kilichorejewa katika kanuni ndogo ya (1), yatalipwa na mtu aliyesababisha kizuizi, hatari, uchafuzi au kero hiyo.

(3) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2) mtu anayesababisha kizuizi, hatari, uchafuzi au kero hiyo anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Upuliziaji wa dawa ya kuua wadudu kwenye chombo

160. Mmiliki au nahodha wa chombo hataelekeza chombo kupuliziwa dawa ndani ya mipaka ya bandari isipokuwa kwa kibali cha maandishi cha Nahodha Mkuu wa Bandari na kwa masharti ambayo Nahodha Mkuu wa Bandari anaweza kuweka kwa maslahi ya usalama na utendaji wa weledi na ufanisi wa bandari.

Cheche, masizi, na upakaji rangi

161.-(1) Mmiliki au nahodha wa chombo kilicho bandarini atachukua tahadhari zote za lazima ili kuepuka utokaji mwingi wa cheche, mafusho, masizi, moshi au rangi kutoka kwenye chombo hicho.

(2) Madai yoyote ya uharibifu unaosababishwa na utoaji wa cheche, mafusho, masizi, moshi, au rangi kutoka kwenye chombo yatalipwa na mmiliki au nahodha wa chombo.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2), mtu anayesababisha cheche, masizi, moshi, au rangi ndani ya bandari anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi kiasi cha dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Maji ya farumi

162. Ujazaji au umwagaji wa maji ya farumi hautafanyika ndani ya bandari, isipokuwa kwa ruhusa ya Nahodha Mkuu wa Bandari na chini ya masharti ambayo Nahodha Mkuu wa Bandari anaweza kuweka kwa maslahi ya usalama na utendaji wa weledi na ufanisi wa bandari.

Katazo la umwagaji maji taka

163. Nahodha wa chombo hatamwaga-

(a) maji taka kwenye maji ya bandari au sehemu yoyote ya eneo la bandari isipokuwa kwa ruhusa ya Nahodha Mkuu wa Bandari katika kifaa kilichowekwa kwa ajili hiyo;

(b) mabaki ya maji taka katika bandari yatokanayo na usafishaji wa falka au tanki bila kibali cha maandishi cha Nahodha Mkuu wa Bandari:

Isipokuwa kwamba, Nahodha Mkuu wa Bandari anaweza kuweka masharti anapotoa ruhusa chini ya kanuni hii.

Zuio la uchafuzi na uhifadhi wa mazingira

164.-(1) Mtu aliye ndani ya bandari atachukua hatua zote zinazofaa kuzuia, kupunguza na kuondoa madhara ya uchafuzi au uharibifu wa mazingira.

(2) Mtu anayechafua, anayeharibu au anayesababisha uharibifu wa mazingira atabeba gharama zinazohusiana na kurejeresha na kusafisha uchafuzi au uharibifu huo, na athari zinazohusiana nazo.

(3) Endapo mtu anayehusika na uchafuzi au uharibifu wa mazingira atashindwa kuchukua hatua zinazohitajika kuzuia, kupunguza, kuondoa madhara, kurejeresha na kusafisha uchafuzi au uharibifu wa mazingira, pamoja na athari zake, Mamlaka inaweza kuchukua hatua zinazohitajika kukabiliana na uchafuzi huo.

(4) Gharama na madai yatakayoingiwa na Mamlaka kama ilivyorejewa katika kanuni ndogo ya (3), yatalipwa na mtu huyo.

Miundombinu ya kupokelea taka bandarini

165.-(1) Mwendeshaji wa kituo na nahodha wa chombo watatumia vifaa vya bandari kwa ajili ya kuhifadhia taka kutoka kwenye chombo.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kumtaka -

(a) mwendeshaji wa kituo kutoa au kununua vifaa stahiki na vya kutosha kutoka kwa mtoa huduma wa utupaji taka aliyeidhinishwa kwa ajili ya kuhifadhia taka kutoka kwenye chombo

kinachotumia bandari; na

(b) mmiliki au nahodha wa chombo kutoa au kununua vifaa stahiki na vya kutosha kutoka kwa mtoa huduma wa utupaji taka aliyeidhinishwa kwa ajili ya kuhifadhia taka kutoka kwenye chombo ikiwa huduma hiyo haitolewi na mwendesha kituo.

(3) Katika kutathmini utoshelevu wa vifaa vya kuhifadhia taka vilivyotajwa katika kanuni ndogo ya (2), mwendeshaji wa kituo au mmiliki au nahodha wa chombo, kamaitakavyokuwa, atazingatia Mpango wa Udhibiti wa Taka wa Mamlaka.

(4) Bila ya kujali masharti ya kanuni hii, mmiliki au Nahodha wa chombo atatupa taka kwa mujibu wa Mpango wa Udhibiti wa Taka wa Mamlaka.

Matumizi ya Mpango wa Mamlaka wa Udhibiti Taka

166. Mpango wa Udhibiti wa Taka wa Mamlaka utatumika kwa waendeshaji wa vituo, wapangaji na watumiaji wote wa bandari.

Uondoshaji wa chombo bandarini

167.-(1) Nahodha Mkuu wa Bandari anaweza kuamuru kuondolewa kwa chombo kutoka bandarini iwapo chombo hicho kina shehena au kitu kingine ndani ambacho kinaweza kuwa hatarishi kwa mazingira kwa gharama za mmiliki au nahodha wa chombo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) Nahodha Mkuu wa Bandari anaweza kuamuru shehena au kitu kingine kuondoshwa, kwa gharama ya mmiliki au nahodha.

Udhibiti wa wanyama, ndege, samaki na mimea

168.-(1)Mtu hatakusanya, hatatumia, hataondoa au hatahamisha mnyama, ndege, samaki au mmea wowote ulio ndani ya eneo la bandari isipokuwa kama ameidhinishwa na Mamlaka.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya kwanza hatatafsiriwa kuwa yanaathiri leseni, makubalia au upangaji ambao umeingiwa na Mamlaka kwa ajili ya kudhibiti wadudu.

Maziko bandarini

169. Mtu hatazika au kutupa maiti au mzoga wa

aina yoyote ndani ya mipaka ya bandari.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## ULINZI NA UDHIBITI BANDARINI

Kufunga barabara na gati

170. Mamlaka inaweza, ndani ya eneo lolote la bandari, kufunga barabara yoyote na gati, ghala au sehemu yake yoyote, na inaweza kuruhusu au kuzuia matumizi yake kwa kuzingatia masharti au malipo ambayo Mamlaka itaona inafaa kuyaweka.

Gari kuegeshwa sehemu iliyopangiwa

171.-(1) Gari lililo ndani ya eneo la bandari litaegeshwa katika nafasi au sehemu liliyopangiwa na Mamlaka.

(2) Mtu anayehusika na gari ndani ya eneo la bandari atahamisha gari lake anapotakiwa kufanya hivyo na Mamlaka.

Kuingia bandarini bila kibali

172. Mtu ambaye hajaruhusiwa-

(a) hataingia eneo la bandari, kupanda juu ya paa la ghala au juu ya krini, mnara wa taa, kituo cha mawimbi ya mawasiliano au alama ya kuongozea vyombo; na

(b) hataondoa au hataingiza katika eneo la bandari mbao, ubao, mimea, mchanga, mawe, maji, au makuti.

Uendeshaji hatarishi

173. Mtu aliyeidhinishwa hataendesha gari kwenye njia za ndani ya eneo la bandari kwa namna inayoleta hatari kwa umma.

Mwenendo wa madereva bandarini

174. Dereva au mtu anayesimamia gari wakati wote akiwa ndani au akiwa anaingia au kutoka katika eneo la bandari, ataenenda kwa utaratibu na atatekeleza amri zitakazotolewa mara kwa mara na Mamlaka, pamoja na masharti ya notisi au alama yoyote inayooneshwa na au kwa maelekezo ya Mamlaka.

Uharibifu wa mali za Mamlaka

175. Dereva au mtu anayesimamia gari atawajibika kwa uharibifu wowote utakaosababishwa na kuendesha gari kwa uzembe na Mamlaka inaweza kushikilia gari au

mali yoyote hadi pale gharama hizo zitakapofidiwa au Mamlaka kuelekeza vinginevyo.

Ishara za hatari

176. Mtu aliye ndani ya eneo la bandari hatapuuza ishara ya hatari au kukataa kusimama anapotakiwa kufanya hivyo na Mamlaka.

Katazo la maegesho ya gari

177. Gari haitaegeshwa juu, chini au karibu na bomba la kuzima moto, eneo la gatini, kivuko cha reli au njia za winchi, vifaa vya kuhudumia bandari na eneo lingine lililozuiliwa kama itakavyoelekezwa na Mamlaka.

Kuwa na kitambulisho au pasi

178. Mtu anayeingia katika eneo la bandari ataonyesha kwa uwazi kitambulisho au pasi kuanzia muda wa kuingia hadi muda wa kutoka katika eneo la bandari.

Kuingia na kutoka katika eneo la bandari

179.-(1) Mtu-

(a) hataingia au kutoka nje ya eneo la bandari bila kibali;
(b) ataingia au kutoka katika eneo la bandari kupitia mageti ya kuingilia au kutoka nje yaliyowekwa kwa ajili hiyo na atazingatia amri na maelekezo ya Mamlaka.

(2) Mtu anayetaka kuingia katika eneo la bandari kwa madhumuni halali anaweza kufanya hivyo, kwa kuzingatia masharti kwamba Mamlaka haitawajibika kwa majeraha, hasara, uharibifu, ucheleweshaji au kumweka kizuizini au kuharibiwa kwa mali yake kutakakosababishwa kwa namna yoyote:

Isipokuwa kwamba, masharti ya kanuni ndogo ya (2), hayatatumika kwa watumishi wa Mamlaka.

Katazo la kutoa mzigo bila kibali

180.-(1) Mtu, kwa kujua au kwa kutokujua, hataweka au hatasababisha kuwekwa kwenye gari lolote linalokusudiwa kutumika kwa ajili ya kusafirisha bidhaa nje ya eneo la bandari, au kutoa nje ya eneo hilo la bandari, kifurushi chochote, mfuko au kitu cha aina yoyote ndani ya eneo hilo isipokuwa baada ya kupata, au kupata na kuwasilisha kwa Mamlaka kwenye lango la bandari lililotengwa, kama itakavyokuwa, kibali cha kupitisha mzigo kinachomruhusu mtu huyo kutoa kifurushi, mfuko

au kitu hicho nje ya eneo la bandari:

Isipokuwa kwamba, kupata, au kutoa na uwasilishaji wa kibali hicho unaweza kufanywa kupitia mfumo wa usalama wa kielektroniki.

(2) Kibali cha kupitisha mzigo hakitaidhinishwa baada ya ukaguzi wa shehena iliyooneshwa, mizigo ya abiria na vitu kutoka kwenye chombo ambavyo havijaonyeshwa, isipokuwa na mpaka taratibu zote za forodha zimetekelezwa na ushuru, kodi, na tozo zote za bandari kwa ajili ya mizigo hiyo zimelipwa au kuwekewa dhamana.

(3) Endapo vifurushi, vifungashio au vitu vimetolewa nje ya eneo la bandari kwa njia ya reli, vifurushi, vifungashio au vitu hivyo vitatolewa pale tu vitakapokuwa vimetolewa kwenye vitabu ipasavyo kwa ajili ya kusafirishwa na baada tu ya taratibu zote za forodha kutekelezwa na tozo za bandari zimelipwa au kuwekewa dhamana.

Ufungaji wa mageti ya bandari

181. Mamlaka inaweza, katika mazingira maalum na baada ya kutoa notisi, kufunga mageti ya bandari.

Idhini ya kufanya shughuli ndani ya eneo la bandari

182. Mtu hatafanya shughuli yoyote ndani ya eneo la bandari bila kupata idhini kutoka kwa Mamlaka.

Udhibiti wa wanyamapori na wanyama wasiofugwa

183. Mamlaka itashughulikia wanyama wasiofugwa na wanyamapori wanaopatikana kwenye maeneo ya bandari kwa mujibu wa sheria husika:

Isipokuwa kwamba, wale walio kwenye chombo kilicho ndani ya eneo la bandari watahifadhiwa ipasavyo na Nahodha wa chombo.

Matumizi ya king'ora

184. Mtu hatapiga kingo'ra bila ruhusa ya Mamlaka, isipokuwa kwa madhumuni ya urambazaji au kutoa kiashiria cha moto.

Kibali cha farumi

185. Mtu hatatoa mawe au mchanga ndani ya mipaka ya eneo la bandari bila ya kibali cha Mamlaka na

kwa kuzingatia malipo ya tozo kama itakavyoainishwa na Kitabu cha Tozo.

Katazo la uvutaji sigara

186.-(1) Mtu hatavuta sigara ndani ya eneo la bandari isipokuwa katika eneo lililotengwa kwa ajili hiyo na Mamlaka.

(2) Mtu anayekiuka kanuni hii, bila kujali adhabu nyingine yoyote ambayo inaweza kutolewa chini ya Kanuni hizi au sheria nyingine, anaweza kuondolewa kutoka katika eneo la bandari.

Kamati ya ulinzi bandarini

187-(1) Imeundwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bandari.

(2) Majukumu na muundo wa Kamati ya Usalama wa Bandari yataainishwa chini ya Mkataba wa Usalama wa Bandari.

Ulinzi na uingiaji bandarini

188. Kwa kuzingatia masharti ya sheria yoyote inayosimamia vyombo vya usalama vya dola, Mamlaka itawajibika kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa ulinzi na usalama ndani ya eneo la bandari.

Taratibu za uingiaji kwenye maeneo yaliyodhibitiwa

189.-(1) Mtu-

(a) hataingia kwenye jengo linalodhibitiwa isipokuwa kwa ruhusa ya Mamlaka; na
(b) hatabaki katika jengo linalodhibitiwa baada ya kuamriwa kuondoka na Mamlaka.

(2) Afisa wa usalama wa bandari anaweza kutumia nguvu stahiki kumwondoa mtu ambaye anaendelea kubaki ndani ya jengo linalodhibitiwa au eneo lililozuiliwa kwa kuwa anakiuka kanuni ndogo ya (1)(b).

Ukaguzi

190.-(1) Mtu aliyeidhinishwa atampekua mtu, mabegi, mizigo, gari, chombo au mali nyingine inayohamishika ya aina yoyote inayoingia au inayokaribia kuingia kwenye jengo linalodhibitiwa au eneo lililozuiliwa.

(2) Mtu ambaye-

(a) anakataa kufanyiwa upekuzi; au
(b) anakataa kufanyiwa upekuzi kwa mabegi, mizigo, gari, chombo au mali yake nyingine inayohamishika,

anaweza kuzuiliwa kuingia katika eneo lililozuiliwa au jengo linalodhibitiwa.

(3) Mtu aliyeidhinishwa ambaye ana sababu za msingi za kuwa na mashaka kuwa kitu kilichozuiliwa kimo, au kinaweza kuletwa ndani ya jengo linalodhibitiwa au eneo lililozuiliwa, anaweza kupekua sehemu yoyote ya-

(a) jengo linalodhibitiwa au mizigo yoyote, shehena, gari, chombo au mali nyingine inayohamishika ya aina yoyote ambayo, au mtu yeyote ambaye, kwa wakati huo yuko katika sehemu yoyote ya jengo linalodhibitiwa; na

(b) eneo lililozuiliwa, au mzigo wowote, shehena, gari, chombo au mali nyingine inayohamishika ya aina yoyote ambayo, au mtu yeyote ambaye, kwa wakati huo yuko katika sehemu yoyote ya eneo lililozuiwa.

(4) Mtu aliyeidhinishwa anaweza, wakati anapotumia mamlaka aliyopewa chini ya kanuni ndogo ya (3) na katika mazingira maalum, kuingia kwenye jengo lolote linalodhibitiwa au jengo lolote au miundombinu katika eneo lililozuiliwa au ardhi yoyote katika eneo lililozuiliwa kwa nguvu.

(5) Endapo, wakati wa upekuzi unaofanywa chini ya kanuni hii, kitu kilichopigwa marufuku kitapatikana, mtu aliyeidhinishwa atamkamata mtu mwenye kitu kilichopigwa marufuku na atachukua kitu hicho na atawasiliana na kumfikisha mtu na kitu hicho kwa afisa wa polisi aliye ndani ya eneo la bandari ndani ya saa nane.

(6) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (7), upekuzi unaofanywa chini ya kanuni hii utafanywa hadharani na hautamtaka mtu kuvua nguo isipokuwa koti la nje au jaketi na vikinga mikono na kofia.

(7) Endapo itahitajika kuvua zaidi ya koti au koti la nje na vikinga mikono au kofia ili kuona kama kitu kilichokatazwa kimebebwa, upekuzi utafanywa kwa faragha na mbele ya watu wawili au zaidi walioidhinishwa ambao watakuwa wa jinsia sawa na mtu anayepekuliwa.

kumzuia afisa wa Mamlaka

191. Mtu aliye ndani ya bandari hatamzuia, kumuwekea kipingamizi, kumsumbua, kumtishia au kumuingilia afisa yoyote, mfanyakazi, wakala au mtu

yeyote aliyeajiriwa na Mamlaka katika kutekeleza wajibu wake au katika utekelezaji wa kazi au masuala anayotakiwa kuyafanya.

Uzingatiaji wa Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Miundombinu ya Bandari

192. Mamlaka itazingatia Kanuni za Kimataifa za Usalama wa Meli na Miundombinu ya Bandari kwa ajili ya ulinzi na usalama wa meli na vifaa vya bandari.

Makosa chini ya Sehemu ya Kumi na Saba

193. Mtu anayekiuka masharti ya kanuni yoyote chini ya Sehemu hii anatenda kosa.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## HUDUMA NDOGONDOGO ZA BANDARI

Leseni, kibali au makubaliano ya utekelezaji wa shughuli ndogondogo bandarini

194. Mtu hatafanya-
(a) shughuli za uhudumiaji, upakiaji au upakuaji wa bidhaa;
(b) kazi kama mhudumu wa mizigo;
(c) kazi za uwakala wa usafirishaji wa mizigo; au
(d) shughuli nyingine yoyote inayohusiana na huduma za meli au bandari na miundombinu yake,

ndani ya eneo la bandari bila leseni au kibali halali au makubaliano na Mamlaka na kwa kulipa ada kama ilivyoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

Kutoa huduma ndogondogo ndani ya eneo la bandari

195.-(1) Mtu hatafanya biashara ya kutoa huduma ndogondogo ndani ya eneo la bandari bila leseni hai iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na kulipa ada iliyoainishwa kwenye Kitabu cha Tozo.

(2) Mtu hataingia ndani ya chombo kwa ajili kutoa kwenye chombo, ghala za baharini, kufagia, mabaki ya mbao, miti au kitu kingine, bila ruhusa ya maandishi ya nahodha wa chombo.

Mhudumu wa mizigo bandarini

196. Mhudumu wa mizigo bandarini, wakati wote ambao ndani ya eneo la bandari, ataonyesha kwa uwazi

kitambulisho.

Ufutaji au usitishaji, wa leseni au kibali

197. Mamlaka inaweza kwa maslahi ya utendaji, usalama, ubora na ufanisi wa bandari-
(a) kukataa kutoa au kuhuisha leseni au kibali; na
(b) kusimamisha au kufuta leseni au kibali kilichotolewa chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA TISA
## MASHARTI YA JUMLA

Malipo na tozo za bandari

198. Tozo za chombo, uchukuzi, uhudumiaji, uhifadhi wa mzigo na tozo nyingine za bandari ikijumuisha tozo kwa ajili ya huduma ya utayari ya zima moto kwa mizigo hatarishi zitatozwa kwa viwango kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Tozo.

Makubaliano ya kutoa huduma

199.-(1) Mamlaka inaweza kuingia kwenye makubaliano na mtu yeyote ikijumuisha kampuni au chama chochote au kikundi cha watu au shirika kwa ajili ya kufanya au kutoa huduma au vifaa zinazoweza kufanywa au kutolewa na Mamlaka.

(2) Endapo Mtu aliyerejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), ni taasisi itatakiwa-
(a) ikiwa ni kampuni ya kigeni, angalau asilimia arobaini na tisa ya hisa ziwe zinamilikiwa na rai wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(b) kuwa na mkurugenzi au mbia ambaye ameapa kwamba-
(i) hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa;
(aa) dhidi ya usalama wa nchi;
(bb) udanganyifu, kughushi, rushwa au makosa ya uhujumu uchumi;
(cc) kutolipa au kukwepa kodi yoyote au ushuru unaolipwa chini ya sheria yoyote ; na
(dd) dhidi ya maadili.

Sura ya 25

(ii) haijatangazwa kuwa imefilisika chini ya Sheria ya Ufilisi; na
(iii) hana historia ya ukiukwaji wa kanuni

za ulinzi na usalama za ndani na za kimataifa;

(3) Mkurugenzi au mwenye hisa atajaza hati ya kiapo iliyoainishwa katika Jedwali la Pili ili kuthibitisha kwamba hajatiwa hatiani kwa kosa lililorejewa katika kanuni ndogo (2)(b).

Mamlaka kutoa miongozo

200. Mamlaka inaweza kutoa miongozo ya jumla ili kuwezesha utekelezaji bora wa Kanuni hizi.

Adhabu ya Jumla

201. Mtu anayekiuka masharti ya kanuni yoyote chini ya Kanuni hizi, ambapo hakuna adhabu maalumu iliyotolewa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola mia mbili za Marekani au kiasi sawa na hicho kwa Shilingi za Tanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

kufutwa T.S.Na. 413 la 1991

202. Kanuni za Bandari za Tanzania zinafutwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 195 (1))*

LESENI ZA HUDUMA NDOGONDOGO ZA BANDARI

1. Leseni ya biashara na huduma Majini.
2. Leseni ya kutoa huduma ndogondogo kwenye meli.
3. Leseni za boti na vyombo vya majinina cheti cha msamaha kwa uongozaji wa meli bandarini.
4. Leseni za wahudumiaji mizigo midogomidogo bandarini.
5. Leseni ya meli ndondo kwa matumizi mbalimbali bandarini.
6. Leseni ya kukodisha vyombo na kutia nanga bandarini na wahudumu wa vyombo hivyo.

## JEDWALI LA PILI

KIAPO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 199 (3))*

Mimi, …………………………………………………….., wa S.L.P …..……,…..…..………....., nikiwa mkurugenzi/ mmiliki wa hisa za kampuni ……………………………….ambayo inaomba leseni kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa ajili ya kufanya shughuli/biashara ya......................................................................
………………………………………………………………………………………………
……

NAAPA/ NATHIBITISHA KUWA

1. Nina sifa zote za kuomba leseni kwa ajili ya kuendesha biashara ya ………………………………………….

2. Nimepitia na kuelewa sifa zinazohitajika kwa ajili ya kuomba leseni ya kuendesha biashara ya ………………………………………………………………

3. Nikiwa kama mkurugenzi wa kampuni/mmiliki sijawahi kutiwa hatiani kwa makosa dhidi ya
   a. usalama wa nchi;

b. kutolipa au kukwepa kodi;
c. udanganyifu, kughushi, rushwa au makosa ya uhujumu uchumi; na
d. makosa yoyote ya kimaadili.

4. Nikiwa kama mkurugenzi sijawahi kutangazwa kufilisika kwa mujibu wa Sheria za Ufilisi, Sura ya 25.

5. Nikiwa kama mkurugenzi sina kumbukumbu au sifa yoyote ya kuvunja kanuni za usalama wa nchi au za kimataifa.

6. Nimepewa muda wa kutosha wa kujiridhisha kuhusiana na sifa zinazohitajika, hivyo nitawajibika kwa maelezo niliyotoa hapo juu.

tarehe……………mwezi……….mwaka………………

………………..
MUAPAJI

UTHIBITISHO

Mimi………………… nadhibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kwenye aya ya 1, 2, 3,(a-e), 4, 5, na 6 ni kweli mtupu.

Kimethibitishwa hapa.………………………… tarehe….…… mwezi ……………………. Mwaka 20………

kimeapwa au kutihibitiwa hapa……………………………
na…………………………….
ambaye na mfahamu/ambaye ametambulishwa kwangu na ……….
leo tarehe……………...mwezi wa……………20 …..

……………….

…………………
MUAPAJI

MBELE YANGU

Jina:……………………………………………
saini……………………………………...
Anwani:…………………………………………
Sifa:Kamishaina wa Viapo

Dodoma,
20 Juni, 2024

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Uchukuzi*